

KAMA NILIVYOKUWA

PAMOJA NA MUSA, NDIVYO

NITAKAVYOKUWA PAMOJA NA

WEWE

 Nje tena asubuhi ya leo baada ya usingizi mzuri usiku. Natumaini kuwa sote tulikuwa nao, na tunajisikia kuburudika leo.

² Nilikuwa nikifikiria tu, nilipokuwa nimesimama chumbani, naye Billy Paul akaweka senti ishirini na tano, asubuhi ya leo. Nakumbuka nikisimama kwenye mimbara ii hii, wakati... Frankie Weber, jirani hapa, mimi na yeye tulienda shule pamoja. Na nilikuwa na karibu ishirini na mmoja, na, au, yapata ishirini na miwili, ninaamini. Naye alikuwa tayari na ishirini na mitano. Basi alipoweka senti ishirini na tano, niliwazia, “Loo, jamani! Frankie yuko karibu na kufa! Ni mzee sana!” Na—na sasa... Niliwazia, “Je, nitafanya nini nitakapofikia umri huo, ishirini na mitano?” Na sasa mwanangu anaweka ishirini na tano.

³ Inaonyesha tu kwamba majira yanapita mbio, wala hayamsubiri mtu yeyote. Lazima tufanye kazi kungali mchana, kwa kuwa wakati utakuja ambapo hatuwezi kufanya kazi tena. Na sikuzote nilipenda *Zaburi ya Maisha* ya Longfellow, “Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu kumbukumbu za kudumu.” Hatuna budi kuweka kumbukumbu wakati tunapoweza kuziweka, kila mmoja wetu. Hebu tusipoteze hata siku moja, lakini tufanye kila siku ihesabiwe vizuri tuwezavyo, kwa ajili ya utukufu Wake.

⁴ Siku chache zilizopita usiku, au wiki mbili zilizopita, imekuwa hivyo. Bwana hutoa maono, kama sisi sote tujuavyo hilo hakika hapa. Nami nilikuwa na ono la ajabu lililonitokea nilipokuwa kule chini Kentucky. Nikakiambia kikosi nilichokuwa nacho, “Jambo fulani hakika linakaribia kutukia.”

⁵ Niliona amesimama mbele yangu, yapata saa tisa alfajiri, chumbani, mtu, mweusi vibaya sana; sio kama ndugu na dada zetu weusi wapendwa. Mtu huyu alikuwa tofauti. Mwili wake ulikuwa chuma iliyokunjikakunjika. Naye alikuwa akija na mikono mikubwa iliyokamatana, kunishika. Na kinga yangu ilikuwa wembe mdogo, lakini haukufaa kitu. Usingeniwezesha

kujikinga nao. Kwa hivyo, kwa namna fulani, Bwana aliingia na kunisaidia kutoka kwa mtu huyu wa kutisha. Alikuwa chuma iliyokunjamana. Ningeweza kumwona wakati akiinua mkono wake, makunyanzi makubwa katika ngozi yake, kama tu chuma kikienda huku na huku. Nadhani, labda, risasi ngumu haingeweza kutoboa ganda hilo lenye kutisha, kama mnyama fulani, kobe au kitu fulani, juu yake. Naye alikuwa ananiandama. Nina fununu nzuri hiyo ilikuwa ni nini na inalomaanisha.

⁶ Lakini, basi, Jumanne iliyopita asubuhi, yapata saa tisa, kitu kingine kilitokea. Nilikuwa nyumbani. Ndipo mbele yangu chumbani, alisimama Mtu wa Kiungu ambaye aliongea maneno ambayo sikuelewa. Na wakati aliochagua umekaribia. Wala sikumsikia vizuri sana, lakini alikuwa Mtu wa Kiungu. Naye akasema, “Siku saba zaidi, nawe utasimama kama Musa alivyosimama,” au “utakuwa kama Musa alivyokuwa,” au jambo fulani kuhusu Musa. Hiyo inaniachia siku moja zaidi, baada ya leo. Hiyo ilikuwa ya sita. Sijui hiyo inamaanisha nini. Ninajua kwamba Yeye atalitekeleza, lolote lile. “Utasimama,” au, “itakubidi kusimama,” au, “uwe kama,” au, lilikuwa ni jambo linalohusu Musa. Na mimi sikuliwazia sana. Niliambia familia yangu na kuwaambia wengine, wapendwa wangu, kwamba nilimwona huyu Wa Kiungu. Hata hivyo, alizungumza kama mwanadamu.

⁷ Halafu nikagundua kuwa Ujumbe wangu, wa jana jioni, Bwana alinijalia kumchagua Musa. Na, asubuhi ya leo, ni Musa na halifa wake. Nayo Maandiko ambayo niko karibu kuyaendea, asubuhi ya leo, kwake, yanahusu Musa na Yoshua. Nalo andiko hili, Yoshua sura ya kwanza, daima limekuwa Andiko muhimu sana. Sijawahi kulihubiri, maishani mwangu; nitajaribu, asubuhi ya leo.

⁸ Lakini, yapata miaka miwili iliyopita, niliona Biblia, chumbami, ikishuka na kusimama mahali nilipokuwa. Ndipo Mkono, kutoka juu, ulishuka na kuzitenganisha hizo kurasa, akazifungua; kisha akashuka, Yoshua 1, hadi kifungu cha 9, ndipo akasimama, huku anaenda polepole. Nimeingojea saa hii ikaribie, wakati ambapo ningeishi kwamba ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwangu kulizungumza.

⁹ Sasa, msisahau ibada za jioni, ikiwa mko...mnaweza kuja, na huna mahali pa wajibu. Endapo mna makanisa yanayowahitaji, mbona, bila shaka tunakupendekezea kanisa lako.

Asubuhi ya leo tutawaombea wagonjwa, mara tu baada ya Ujumbe. Nami nadhani, hapo, kufuata huo, ni ibada ya ubatizo.

¹⁰ Basi usiku wa leo, Bwana akipenda, nataka kuhubiri juu ya *Vitambulisho Vitano Vya Kimaandiko Visivyoweza Kukosea, Vya Kanisa*, na uhusiano wetu Nalo, na Kanisa la Agano Jipya,

na uhusiano wetu na Kanisa hili. Na ibada zitaanza, ibada ya wimbo, saa moja u nusu; nitajaribu kuwa mimbarani saa mbili. Nasi tutamaliza kufikia saa tatu u nusu, Bwana akipenda.

¹¹ Halafu basi ninaamini, kwamba, leo, kwamba haitakuwa hata moja ya maneno haya, kwamba, nitakapofika kwenye lile agizo, kwamba hakuna mtu atakayeshindwa kuliona. Kwa sababu, ni muhimu sana kwamba uweke kando kila kitu sasa, na kuwazia, tunapomngojea Roho Mtakatifu.

¹² Kabla ya kukaribia Neno hili zuri sana na la rehema, nitaomba kwamba rafiki yangu mwema na mfanyakazi mwenzangu, Dk. Lee Vayle, iwapo atasimama na kutuongoza kwa maombi mafupi, tunapolifungua Neno. Ndugu Vayle.

[Ndugu Lee Vayle anaanza kuomba. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Asante, Ndugu Vayle, kwa maombi hayo yanayotia moyo kwa Mungu.

¹³ Basi sasa na tuyageukie Maandiko. Kuna mengi tu ya kuzungumziwa; lakini hata hivyo nikiwaona wengi wamesimama karibu na kuta, na kumbini, na kadhalika. Ninaamini tunakabiliwa na mapambazuko ya siku mpya. Sasa, katika kusoma Maandiko asubuhi ya leo, hebu tufungue mlango wa kwanza wa Yoshua. Nasi tutasoma kutoka Kitabu cha kwanza cha Yoshua, mlango wa kwanza, vifungu tisa vya kwanza. Wakati tukijiandaa. . .

¹⁴ Ujumbe huu unarekodiwa, na utatumwa sehemu nyingi za ulimwengu. Ningependa watu wa ulimwengu ambao Bwana amenipa kibali, na nilipata neema machoni penu. Ninasema hivi, asubuhi ya leo, kwa sababu kwamba, katika siku zijazo, natarajia kuja katika kusanyiko lenu na mikutano, ili mjue, mapema, yale Bwana Mungu ametenda, mpate kujua Ukweli. Na kama vile Yesu alivyosema, “Kweli itakuweka huru.”

Tunasoma kutoka kwa Yoshua 1.

. . . baada ya kufa kwake Musa, mtumishi wa BWANA, BWANA akamuambia Yoshua, mwana wa Nuni mtumishi wa Musa, akasema,

Musa mtumishi wangu amekufa; haya basi, ondoka, kisha vuka mto huu wa Yordani, wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi ambayo nimewapa wana wa Israeli.

Kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu, nimewapa nyinyi kama nilivyomwapia Musa.

Tangu jangwa hili na mlima huu, Lebanoni, mpaka mto ule mkubwa, mto wa Frati, nchi yote ya Wahiti, . . . mpaka bahari ile kubwa upande wa machweo ya jua, hapo ndipo patakapokuwa mpaka wenu.

Hapatakuwa na mtu yeyote atakayeweza kusimama mbele yako siku zote za maisha yako: kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe: sitakupungukia wala sitakuacha.

Uwe hodari na moyo wa ushujaa: maana ni wewe utakayewarithisha watu hawa nchi hii niliyowaapia baba zao ya kwamba nitawapa.

Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote, aliyokuamuru Musa mtumishi wangu: usiache, kwenda mkono wa kuume au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako.

Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako; bali utayatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo: maana ndipo utakapozifanikisha njia zako, kisha ndipo utakapositawi sana.

Je, si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike: kwa kuwa BWANA, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.

¹⁵ Na katika kifungu cha 5, na karibu katikati ya huo mlango, imeandikwa: *Kama Nilivyokuwa Pamoja Na Musa, Ndivyo Nitakavyokuwa Pamoja Na Wewe*. Hilo ndilo, kama ningeliita somo, ningependa ku—kusubiri kwa dakika chache, na kuvuta usikivu wenu kwenye hilo. “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.”

¹⁶ Sasa jana jioni tulikuwa tukisafiri pamoja na wana wa Israeli, kote kutoka Misri, hata tukawafikisha Kadeshi. Loo, ni somo zuri jinsi gani! Ni jambo kubwa jinsi gani, tulipokuwa tukifananisha kanisa la kawaida na kanisa la kiroho. Mungu akishughulika na Israeli kwa kawaida; pamoja na kanisa katika siku hizi, anapoita kutoka kwa Mataifa, watu kwa ajili ya Jina Lake. Anashughulika nao katika mambo ya kiroho, kama alivyoshughulika nao kwa mambo ya kawaida; sambamba tu, moja kwa lingine. Na yote ambayo Mungu alifanya nao, na yote ambayo Mungu aliwafanyia, na yote waliyofanya kujibia, yanatuangukia kama mfano. Nasi tunaona, umbali huu, Neno limetekelezwa vivyo hivyo hasa. Jinsi ambavyo kwa kawaida, walipopata ushindi wao mara moja au mbili, walishikilia kushangilia, na kupiga makelele, na kucheza, na kumsifu Mungu; vile tu kanisa lilivyofanya, na sasa limesubiri miaka arobaini kwa ajili ya kufunguliwa kwa kitu kingine.

¹⁷ Na wakati tukifikiria juu ya Musa, mtumishi huyu mkuu wa Bwana, jinsi ambavyo wakati wa kuzaliwa kwake, mahali alipozaliwa, Mungu alimchagua kwa kazi yake, wakati wa kuzaliwa kwake. Na maisha yake yalikuwa magumu sana kuishi. Kwa sababu, yeye ni mtu, na anataka kuishi kwa njia moja, naye Roho wa Mungu anamwongoza njia nyingine. Ni maamuzi ya

kipumbavu jinsi gani, inaonekana, ambayo angefanya. Wakati, huku mguu mmoja ukiwa juu ya kiti cha enzi, apate kuwa mrithi wa ulimwengu; halafu achukue upande huo mwingine, kuwa mtengwa, au mzururaji. Inaonekana, kiakili, lingekuwa jambo la kipumbavu.

¹⁸ Lakini tunapata somo kubwa humu. Kwamba, watu wanaomfuata Roho, ni wapumbavu, kwa ulimwengu, kwa sababu wao ni wa Ufalme mwingine, wakiongozwa kwa njia nyingine, wakiongozwa na Roho. Mungu jalia hiyo iwe ni mimi, na ninyi nyote, kwamba tutafuata mwongozo wa Roho, haidhuru, tukiangalia ahadi ya Mungu, tukiingojea itimie.

¹⁹ Na hivyo ndivyo tu Musa alivyofanya. Farao alisoma Andiko lile lile ambalo Musa alisoma. Ila tu, Farao aliliangalia kwa njia nyingine. Musa aliwatazama watu wale wale ambao Farao aliwatazama. Farao aliwaona kama watumwa na kama wakanyaga matope. Musa aliwaona kama walioitwa na waliochaguliwa.

²⁰ Hivyo ndivyo ninavyotaka kuliona Kanisa la Mungu aliye hai, sio kundi la walokole au waliotengwa, lakini kama wateule wa Mungu; ili niweze kutoa maisha yangu, kama Musa alivyofanya, kwa ajili ya Kanisa hili kuu na kwa Huduma.

Sasa, tunapata Musa akiitwa. Na baada ya kuagizwa, alishindwa agizo lake, kwa kujaribu kulifanya kwa njia ambayo alifikiri ilikuwa bora zaidi.

²¹ Kwa hivyo inatufundisha, tena, kwamba hatuwezi kuchukua kile tunachofikiria ni bora zaidi, au kile mwanadamu anafikiria ni bora zaidi. Inatubidi kuchukua njia ambayo Mungu amesema ni bora zaidi. Kwa hivyo, kufuata Neno la Bwana ni bora kila wakati. Chukua njia aliyosema Mungu.

²² Na katika kushindwa kwake, tunaona kwamba alikimbia kutoka mbele ya Farao, akaenda nyikani, ambako alimwoa binti ya Yethro, Zipora. Na huko, baada ya kumwoa, alimzalia mwana, Gershomu. Kisha akatulia, kwa utulivu na kwa amani, katika shughuli ya kondoo.

²³ Lakini, siku moja, Mungu alisikia kilio cha watu Wake. Mungu alikumbuka kwamba alikuwa na agano na watu hao. Isitoshe, bali pia alikumbuka alikuwa na mtumishi ambaye alikuwa amemwita, naye alikuwa amemchagua, na alikuwa na agano na mtumishi huyo. Na Mungu kamwe hatalibadilisha agano Lake au kubadilisha matakwa Yake, au kubadilisha kitu chochote. Mungu daima atatimiza ahadi Zake. Ingawa Musa alikuwa amemkosea na alikuwa amefanya kosa, hata hivyo Mungu alitimiza agano Lake. Mungu anapomwita mtu kufanya jambo fulani, lazima alifanye, hana budi tu kulifanya.

²⁴ Mtu mmoja aliniuliza, siku moja, “Je, tutafute karama zetu sasa kwa ajili ya huduma zetu?” Ndugu fulani wa Kimethodisti ambao walikuwa ndio kwanza wampokee Roho Mtakatifu.

Nikasema, “Hapana. Msifanye hivyo. Mnapofanya hivyo, basi Mungu hawezi kuwatumia.” Nilisema, “Jambo pekee la kufanya, ni kuendelea tu kuwa Mkristo. Ikiwa Mungu amekuita, Yeye atakuweka mahali pako haswa.”

²⁵ Kwa kawaida, wale wanaotafuta na kujaribu kupata vitu, kama Mungu angewapa kitu, wangukuwa, takriban, wenye kiburi. Kwa kawaida, mtu ambaye Mungu anamwita, ni yule mtu anayejaribu kumkimbia, kwa vyovyote vile; Musa na Paulo, na wengineo, wakijaribu kuukwepa wito.

²⁶ Lakini tunaona hapa kwamba, Mungu, licha ya makosa yote ambayo Musa alikuwa amefanya, bado alikuwa ameweka mkono Wake juu yake. Naye akamwita aende, akafanye huduma Yake, akamwita kwenye agizo lake. Basi ni faraja ya jinsi gani hapana shaka hiyo ilikuwa kwa Yoshua, alipomsikia Mungu akisema, “Kama vile nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.”

²⁷ Ingawa, ikiwa ninajaribu, na nishindwe, Mungu hataniacha. Kamwe sina matumaini sana katika mtu yeyote ambaye anaogopa sana kufanya lolote. Afadhali nipatikane nikishindwa kuliko kuwa mvivu sana kujaribu.

²⁸ Wakati mmoja ilisemekana kwamba Kampuni ya Unga ya Ballard na Ballard iliajiri mtu, naye alikuwa akienda kuandika jina lake, naye mtu huyo hakuwa na kifutio mwishoni mwa penseli yake. Ndipo Bw. Ballard akamwambia, akasema, “Kwa nini huna kifutio?”

Akasema, “Mimi sikosei.”

Akasema, “Basi siwezi kukutumia. Kwa sababu, ukifanya makosa, wewe... Usipofanya makosa, hutafanya chochote.” Hiyo ni kweli.

²⁹ Mungu hakuwajibishi kwa makosa yako. Anakuwajibisha kwa dhambi yako ya kukusudia. “Yeye atendaye dhambi makusudi, akiisha kuupokea ujuzi wa ile Kweli.” Lakini mtu ambaye atafanya kitu, atakosea, ataanguka. Atakosea. Lakini ikiwa kweli ameitwa na Mungu, naye Mungu yuko moyoni mwake, atasimama tena.

³⁰ Walikuwa, wakija kanisani hapa, miaka mingi iliyopita, na huenda wakawa hapa asubuhi ya leo, maskini mwanamume mmoja na mkewe. Walizoea kuimba wimbo ulionichangamsha. Unasema kitu kama hiki:

Nisamehe, Bwana, na unijaribu mara nyingine
tena,
Nitakuwa Wako iwapo Wewe utakuwa wangu;
Nikianguka ama nikishindwa, jalia nisimame
na kujaribu tena,
Nisamehe, Bwana, na unijaribu mara nyingine
tena.

³¹ Ninapenda hilo. Kwa maana, askari yeyote mzuri anaweza kujeruhiwa au kuumizwa. Lakini kama angali ni askari, na ana lengo, na kitu cha kupigania, atainuka na kujaribu tena. Na askari yeyote mzuri wa Msalaba atafanya vivyo hivyo.

³² Basi kwa Yoshua, amiri jeshi mpya, baada ya Musa kuaga dunia, alipoona kwamba Mungu alikaa naye katika makosa yake, alishikilia agizo lake.

³³ Haidhuru Musa alifanya nini, ilikuwa ofisi ya Musa ndiyo Mungu aliiheshimu. Alikuwa nabii. Alikuwa juu ya manabii wote. Alikuwa kweli zaidi ya nabii yeyote waliyekuwa naye. Wakati dada yake mwenyewe alipomcheka, kwa kuoa msichana wa Kushi, Yeye aliwaita pamoja na kusema, “Je, hamumwogopi Mungu?” Kasema, “Akiwapo mtu miongoni mwenu, ambaye ni wa kiroho au nabii, nitazungumza naye katika maono na kujitambulisha kwake katika ndoto. Lakini sivyo ilivyo kwa Musa; ninanena naye mdomo kwa sikio. Je, hamumwogopi Mungu?”

³⁴ Mnaona, hilo si jambo zuri, kuwakanyaga watu wa Mungu. Unamuudhi unapofanya hivyo. Mungu alikuwa amemwamuru Musa; kushindwa kwake hakukumaanisha lolote. Mungu aliujuua moyo wake.

³⁵ Naye wakati mmoja, Musa, alilalamika kuhusu kuwa na kazi nyingi mno za kufanya. Basi kwa hivyo Mungu alichukua Roho Yake na kuigawanya miongoni mwa sabini. Hawakuwa na kiwango zaidi cha Roho kuliko walichokuwa nacho mwanzoni. Lakini jambo la pekee, walikuwa na vyombo vingi zaidi tu, kiwango sawa cha Roho.

³⁶ Mungu anaweza kuweka Roho Wake wote juu ya Mtu akitaka Yeye, ama anaweza kuisambaza kati ya maelfu akitaka Yeye. Siku moja aliweka Roho Wake wote juu ya Mtu aliyeitwa Yesu. Sasa amemtawanya kupitia makanisa Yake, kila mahali. Mungu hutimiza agizo Lake.

³⁷ Sasa Yoshua, yule shujaa mpya. Ni wawili tu waliobaki sasa, ambao wamewahi kuondoka katika nchi ya ahadi; hao walikuwa Yoshua na Kalebu. Sasa, Yoshua, yule jemadari mpya, kuliongoza jeshi, kuingia mahali ambapo mtu mkuu kama Musa alisimama. Haikuwa ni kazi rahisi.

³⁸ Nami nawazia juu ya mhudumu, leo hii, aliyeitwa na Mungu, kuingia kwenye njia ambazo Yesu alisimama. Ni amri iliyoje! Ni agizo la jinsi gani! Lakini kila aliyeitwa na Mungu ameagizwa kusimama mahali papo hapo. “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa safari.” Kila mhudumu ameitwa kusimama mahali Yeye aliposimama. “Kazi nifanyazo ninyi nanyi mtazifanya.” Kila mhudumu aliyewekwa na Mungu, ameamriwa kusimama katika njia za Yesu Kristo na kutekeleza majukumu ambayo Yesu alifanya. Hiyo ni amri kuu sana.

³⁹ Na jinsi hapana shaka alihisi, wakati Yoshua alikuwa amesimama pale asubuhi hiyo, akizungumza na Mungu. Alisema, “Sitakupungukia. Na kama vile nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe. Hakuna mtu atakayesimama mbele zako, siku zote za maisha yako. Nitaharibu na kuangamiza. Nitaweka njia wazi. Ila tu, uwe hodari na moyo wa ushujaa. Usifadhaike, hiyo ni, usihofu. Usiogope. Niko pamoja nawe. Nitakufanikisha.” Ni agizo la jinsi gani alilopewa mtu huyu mpya anayelitwa Yoshua!

⁴⁰ Sasa, kuna mifano mingi mno hapa ambayo tungeiendea, lakini tutaruka mingine. Kwa mfano, kama vile Musa, ilikuwa ni wakati wa kanisa uliowaleta Sinai, kwa theolojia yao; ya jana usiku. Musa hakuruhusiwa kuwapeleka wana wa Israeli katika nchi ya ahadi, kwa sababu alikuwa ameshindwa.

⁴¹ Na shirika la kanisa, dhehebu limeshindwa. Hawatalivusha Kanisa. Mungu atainua mfumo mpya, mfumo usioegemea kwenye madhehebu, kwa uweza wa Mungu, ambao utalipeleka Kanisa katika Nchi ya ahadi. Mashirika na madhehebu yamelivuruga, kila moja linafuata theolojia yao wenyewe, kila moja kwa njia yake ya kuwazia. Lakini Mungu atachukua Roho Wake Mtakatifu na atainua akina Yoshua Wake ambao watalipeleka Kanisa kwenye ile ahadi, bila nyuzi za kimadhehebu zilizofungiwa popote, lakini watalivusha Kanisa Lake.

Musa alikuwa ameshindwa; yeye alikuwa mtoa sheria. Yoshua aliitwa kwa neema, naye akalipeleka kanisa mbele.

⁴² Tunapata pia kwamba Yoshua, akijua agizo hili, akijua kwamba lilikuwa mikononi mwake, kwamba Mungu alikuwa amemwitia jukumu ambalo hakupaswa kulipungukia, alienenda kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Ndipo alipowakusanya watu pamoja na kuwaambia kwamba Mungu alikuwa amemtuma, angalia ombi la hao watu. Walisema, “Tutakufuata kama tulivyomfuata Musa, ikiwa tunaweza kuona kitu kile kile kilichomfuata Musa, kikikufuata wewe. Uwe tu hodari na moyo wa ushujaa.”

⁴³ Hayo yanapaswa kuwa ndiyo masharti ya kila mtu aliyezaliwa mara ya pili leo hii. Ikiwa tumeombwa kufuata, basi hebu tuone ishara zikimfuata mwaminio. Kama Yesu alivyosema, “Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya.”

⁴⁴ Nami nimekuomba, hapo awali, uhakikishe umeuacha moyo wako wa kiroho wazi asubuhi ya leo, maana ninatumaini kwamba utashika kile ninachosema. Tukiketi na watu wa madhehebu, kila mamna ya mashirika yamekusanyika hapa asubuhi ya leo, kutoka kwa Katoliki na Protestanti, na aina nyingi tofauti, kwa hiyo itafunuliwa waliojazwa na Roho, bila shaka.

⁴⁵ Sasa ilibidi Yoshua achukue amri hii. Hao watu walisema, “Hebu Mungu awe pamoja nawe kama alivyokuwa pamoja na Musa, ndipo tutajua kwamba Roho yeye yule aliyetuongoza umbali huu anaweza kutupeleka.”

⁴⁶ Loo, jinsi Kanisa linavyopaswa kuangalia, asubuhi ya leo, kumwona Roho akifanya kazi miongoni mwa watu, ikiwa unataka kanisa la nyumbani ambapo Roho aliyemfufua Kristo katika wafu, Roho Mtakatifu, ambaye atatenda kazi miongoni mwa watu. Huyu ni Roho ambaye Mungu anamwinua, katika siku za mwisho, kuwavusha watu, kuingia katika ile Nchi nyingine, katika ahadi kamili ya baraka zote za Mungu, na kwa agizo kamili ambalo Yeye alitoa, au ahadi. “Ahadi hiyo ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu.” Kama Israeli walivyoitafuta hiyo nchi ya ahadi, wakijua ya kwamba ilikuwa mahali fulani, kwa sababu kulikuwako na mtu kule, hapo awali, vivyo hivyo na Kanisa pia. Tunajua kwamba kuna Nchi mahali fulani. Kuna nguvu mahali fulani, kwa sababu kumekuwa na wengine huko. Tunajua kwamba Nchi hiyo iko ng’ambo ya mto, ambapo tunaelekea, asubuhi ya leo, tukijaribu kwenda kwenye Nchi hiyo ya ahadi.

Yoshua alijua kwamba nchi hiyo ilikuwako. Alikwenda kwanza akaipata, apate kurudi kama shahidi.

⁴⁷ Wahudumu walioitwa na Mungu hawapaswi kushindiliwa sana kwa theolojia, bali waitembelee ile Nchi tunakoenda, wakirudi na ushahidi wa upendo wa Kiungu na nguvu za Yesu Kristo, kuyafahamisha makusanyiko yao, kwamba kuna Nchi ng’ambo ya mto.

⁴⁸ Sasa, jana usiku, nikihubiri, “kwenda mpaka Yordani.” Sasa, tukifika kwenye huo mto, unatugawanya. Unatutenganisha. Mara ukiwa kwenye ng’ambo ya pili, jambo fulani limekupata.

⁴⁹ Sasa, Yoshua, katika haya yote, akijua ya kwamba ile amri ilikuwa kuu; bali, akiwa na hakikisho, aliweza kuwa bila woga. Angeweza kuwa, kama tusemavyo, asiyejali, maadamu alikuwa ameelekezwa njia sahihi. Huenda akajitupa dhidi ya kilima ambacho kingemrusha nyuma, lakini alibebwa katika njia sahihi.

⁵⁰ Kwa hivyo Kanisa la Mungu aliye hai linaweza kuwa lisilojali na lisiloogopa, katika imani, ikiwa tumelekezwa njia sahihi. Kwa maana, Yeye alisema, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, nitakuwa pamoja nawe. Sitakuacha wala sitakupungukia.” Yeye kamwe hakumwacha Musa. Hakumpungukia Musa. Hatampungukia Yoshua. Hatatupungukia sisi. Atakuwa pamoja nasi.

⁵¹ Na tunapomwona Yoshua akichukua agizo hili, tukijua kuwa majukumu yalikuwa yakiwaongoza kupitia nchini, sasa, kwamba ingebidi kuingia katika hiyo nchi nyingine. Ingemlazimu kuanzisha ufalme wao. Angelazimika kugawanya

urithi miongoni mwao. Alijua agizo hilo lilikuwa kubwa sana, zaidi ya kile Musa alikuwa amefanya. Yoshua alikuwa na mengi ya kufanya kuliko Musa.

⁵² Jambo lingine, alikuwa awaongoze mpakani, miongoni mwa ndugu zao. Nao tayari walikuwa wameonja damu. Ilimbidi awashinde. Ilimbidi kuwanyamazisha wakati wakisonga mbele taratibu.

Ndivyo ilivyo leo hii na kundi hili jipya la Kipentekoste linaloinuka sasa, wameonja umadhehebu. Ni vigumu sana kuwanyamazisha.

⁵³ Miaka kadhaa iliyopita, walisema, “Njoo, Ndugu Branham,” wakati huduma ilipoanza, “tutaanzisha shirika, tukujengee kumbukumbu mahali fulani.” Sitafuti kumbukumbu. Ninakutafuta kule Kuja kwa Bwana.

⁵⁴ Waliunda dini ndogo potovu, iitwayo “mvua ya vuli,” ikaingia Canada, kisha ikaenda California, lakini ilisambaratika. Bila shaka, haiwezi kwenda. Kwa nini ilikuwa hivyo? Kitu pekee wajuacho; walitoka kwenye vitu hivyo, nao wakakigusa kidogo. Inawabidi kuwa na kitu wanachopaswa kufanya.

⁵⁵ Ndugu, Kanisa halisi la Mungu aliye hai halina itikadi, halina kanuni za imani. Linaongozwa na nguvu za Mungu zilizo ndani ya moyo wa kila mtu. Pita karibu na ndugu zako. Usiwasumbue. “Sisi ni wakuu kuliko wao.” Usibishane nao. Pita tu.

⁵⁶ Nataka muone jambo kubwa lililofanyika hapa. Kulikuwako na Esau, Moabu, na wale tuliowataja, jana usiku. Wengi wa watu hao, wengi wa hao hasa walikuwa waaminio wakwamia mpakani. Walikuwa papo hapo mpakani.

⁵⁷ Loo, sina budi kusimama hapa juu ya jambo fulani kwa muda kidogo tu, haitanichukua ila dakika moja. Watu wengi huilinganisha nchi ya ahadi na ule Utawala wa Miaka Elfu. Sio. Nchi ya ahadi ilikuwa na vita na mauaji. Ule Utawala wa Miaka Elfu hautakuwa na vita vyovyote wala mauaji. Unalinganishwa na Roho Mtakatifu, viwanja vya vita.

⁵⁸ Kuhesabiwa haki; walitoka Misri. Kuna hatua tatu za safari yao. Waliondoka Misri, chini ya kuhesabiwa haki, wakiadini Neno. Wakajitenga na Wamisri na kutoka. Walivuka Bahari ya Shamu na kuua vitu hivyo nyuma yao, ambao ulikuwa ni utakaso kupitia Damu, kunakoua tamaa zote mbaya za kibinadamu; hatua ya pili ya hiyo safari. Lakini hatua ya tatu ilikuwa ni wakati walipovuka Yordani, kuingia nchi ya ahadi ambapo urithi wao ulikaa. Urithi wao haukuwa Misri, ingawa Mungu aliwabariki huko Misri.

⁵⁹ Ninyi Walutheri mnaoamini kuhesabiwa haki; urithi wenu hauko huko, iwapo umeitwa. Ikiwa wewe ni Mlutheri tu, huo ndio umbali utakaopata kwenda.

⁶⁰ Ninyi Wamethodisti, na Wanazarayo, na Pilgrim Holiness, na Church of God, mnaoamini katika utakaso, kuuawa kwa uovu ulio ndani yenu, kuondoa mashina ya uovu, ninyi ni wa ng'ambo ya mto.

⁶¹ Lakini kwenu ninyi wanaume na wanawake mlio na kitu fulani ndani yenu, kinachoita, kilindi kwa Kilindi, kungali kuna Yordani ya kuvukwa, na Nchi ng'ambo ya mto.

⁶² Kasema, "Mtapitia karibu na ndugu zenu. Mtapitia karibu na ndugu zenu, nao wako karibu na mpaka. Mkipitia karibu nao, msiwaambie chochote. Nimempa Esau mlima huu. Nimempa Moabu nchi hii. Wala sitaki mzoane nao, kuwaongoa. Piteni tu, polepole. Mnajua mnakoenda. Msichukue tabia zao."

⁶³ Moabu walikuwa na nabii wa uwongo, askofu aliyetwa Balaamu, ambaye alishuka akaingia miongoni mwa lile kusanyiko, na kujaribu kuwafanya waunde dhehebu, na wote waungane, maana walikuwa ndugu. Lakini hawakuwa hivyo. Walikuwa ndugu nusu, sio ndugu halisi. Ikiwa moyoni mwako...

⁶⁴ "Msibishane naye. Endeleeni tu, achana naye. Gharamia utakachopata, ikikubidi upitie nchini mwake." Alikusudiwa tangu zamani kuwa hivyo. Kama Mungu angalitarajia au kumkusudia Moabu tangu zamani kujiunga na Israeli, wangiungana. Kama alikuwa amemchagua Esau tangu zamani kuambatana na Israeli, Esau angaliruka ndani na kwenda. Lakini Yeye alimpa urithi wake ng'ambo ya mto.

⁶⁵ Kwa hiyo unawezaje kujaribu kuwafanya Walutheri wote kuliona Hilo, Wabaptisti wote kuliona Hilo, Wapresbiteri wote, na Wanazarayo, na Pilgrim Holiness? Usiwahukumu. Hayo ndiyo yote wajuayo. Hayo ndiyo yote yaliyo ndani yao.

⁶⁶ Lakini kwako wewe unayeamini (Ee Mungu!), kwako wewe unayejua, kwako wewe uliye na kitu ndani yako, ambacho kinaita Kilindi. Ikiwa kilindi chote ulicho nacho kimeridhishwa, basi kaa mahali ulipo. Lakini kwangu mimi na nyumba yangu, kwangu mimi kuna kitu zaidi ya kile ambacho tumeona. Kunayo Nchi ng'ambo ya mto, mahali fulani. Kungali kuna kilindi kinachoita Kilindi. Siwezi kuridhishwa na theolojia. Siwezi kuridhishwa na kanisa zuri. Siwezi kuridhishwa na kampeni nzuri. Siwezi kuridhishwa na huduma ndogo ya uponyaji. Kuna kitu zaidi ya hayo, kinachoita.

⁶⁷ Kwa hivyo, achaneni tu nao. Piteni moja kwa moja. Msibishane nao. Lakini tunapita kwenda kwenye Nchi nyingine. Hawakukusudiwa kuambatana nanyi. Hawatatembea pamoja nanyi. Je, watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana? Lakini kwa wale wanaompenda

Mungu, kwa wale walioitwa na Mungu. Vema, wanasema, “Mungu alitupa kanisa hili. Mungu alifanya *hili*.”

Hiyo ni kweli. Mungu alisema, “Nimempa Esau mlima huu. Msimguse. Lakini nina kitu tofauti kwa ajili yenu. Vukeni.” Amina.

⁶⁸ Hiyo ndiyo shauku yangu, ndugu, kuona kanisa langu likivuka kuingia kwenye Nchi nyingine, shauku ya kuvuka hata ng’ambo ya pili. Ikiwa kuna kitu ndani yako, *hapa*, kwanza, kikiita, kutakuwako na Kitu cha kuitikia wito huo. Kutulia tu kwenye ufugaji wa kondoo, hakutoshi kwako. Kuingia katika aina fulani ya biashara, hakutoshi kwako. Kujiunga tu na kanisa na kuandika jina lako kwenye kitabu, hakutoshi kwako. Kwa sababu, kuna kitu kinachoitwa, ng’ambo ya kilima huko, ng’ambo ya kilima cha pili, na kote kuvuka Yordani, mpaka utakapoiangukia mikono ya Mungu, huko ng’ambo, kilindi kikiita Kilindi.

⁶⁹ Yoshua alijua agizo hili lilikuwa ni kuu sana. Mliona pale? “Mimi. . .” Hapo Yoshua alipoanza kuvuka Yordani, jinsi ambavyo Yoshua alikumbuka agizo lake! “Kitabu hiki cha torati, Neno Langu, kisiondoke kinywani mwako.” Kwa maneno mengine, “Yoshua, sijali kabila linasema nini, makasisi wote wanasema nini. Dumu pamoja na Neno hili, maana hapo ndipo utakapozifanikisha njia zako. Haijalishi wanafanya mambo makubwa mangapi, na wanafanya mambo madogo mangapi, na waliunda madhehebu mangapi, dumu pamoja na Neno, Yoshua.” Loo, jamani! “Dumu pamoja na Neno, Neno hili. Neno hili lisiondoke kinywani mwako.” Hebu nilisome tena.

*Uwe hodari na ushujaa mwingi, upate kuangalia
kutenda sawasawa na hayo yote ambayo, sheria yote
aliyokuamuru Musa mtumishi wangu: usiiache, kwenda
mkono wa kuume au wa kushoto, . . .*

⁷⁰ Kama Neno linasema, “Fanya jambo fulani,” lifanye. Sijali shirika linasema nini. Litekeleze, kwa vyovyote vile. Huyu ndiye Yoshua ambaye Mungu anamngojea. Usigeuke inchi moja, hata nukta moja. Dumu moja kwa moja na Neno.

*. . . usiiache, kwenda mkono wa kuume . . . au wa
kushoto, upate kufanikiwa . . .*

⁷¹ Loo, mnafikiri mnafanikiwa wakati mnapojenga makanisa makubwa, kuongeza elfu kumi kwenye dhehebu lenu. Huo sio ufanisi. Hiyo haiwapeleki hatua moja karibu na ile ahadi. Tunachohitaji ni Mungu zaidi, Roho Mtakatifu zaidi.

. . . upate kufanikiwa kila uendako.

*Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako;
bali utayatafakari maneno yake mchana na usiku, . . .*

⁷² Unapowazia kufanya jambo fulani, je, unachukua Neno la Mungu kwa ajili yake? Je, unapata shauku yako katika Neno? Je,

unahubiri yale yaliyo Biblia? Je, wewe ni kama tu wengi siku hizi, na wengi kupita kiasi, “Wanaohubiri Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu”?

Kitabu hiki cha torati kisiondoke mkononi mwako, ama, kinywani mwako; . . .

“Kinywani mwako,” yale usemayo. Usikisome tu na kuondoka. Kinene. Kiishi. Kifundishe.

. . . bali utayatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kutenda sawasawa na yote yaliyoandikwa ndani yake: . . .

⁷³ Mnaona Yoshua wa siku hizi atakavyokuwa? Mnaona jinsi Yoshua wa Kanisa la kiroho atakavyokuwa? Ni Yoshua wa namna ile ile waliyekuwa naye katika lile kanisa la kawaida. Kanisa la kiroho halina budi kuwa kitu kile kile.

Ikiwa Biblia ilisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona Ufalme wa Mungu,” Yoshua wa kiroho atasema, “Amina.”

Kama Biblia ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana na milele,” Yoshua wa kiroho atasema jambo lile lile: “Yeye ni yule yule.”

⁷⁴ Kama Biblia inasema, Kitabu, Neno linasema, kwamba, “Ngojeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mpatakapovikwa uwezo utokao juu. Roho Mtakatifu akiisha kuwajilia juu yenu, ndipo mtakapokuwa mashahidi Wangu,” Yoshua wa kiroho anasema jambo lile lile.

⁷⁵ Kama vile Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, alivyosema, “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu,” Yoshua wa kiroho kamwe hatatofautiana hata nukta moja, bali atafanya yale hasa Neno liliyosema.

⁷⁶ Kama Marko 16 ilisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya,” Yoshua wa kiroho atasema jambo lile lile. Atatafakari hayo mchana na usiku, ili kuifanikisha njia.

⁷⁷ Nataka muone kilichofanyika. Yoshua, alipokuja kwenye uamsho wake wa kwanza, mara yake ya kwanza kuthibitisha kwamba alikuwa Yoshua halisi. Israeli walipaswa kujua hayo.

Bila shaka, makasisi walikuwa na wazo tofauti. Walisema, “Sasa tutapiga kambi hapa mpaka majira ya kuchipua, au mpaka majira ya kiangazi, Yordani itashuka.”

Basi ilionekana kana kwamba Mungu anatupa baadhi ya vitu vya kijinga sana mbele ya Yoshua wa kiroho.

Akamleta huko mwezi wa Aprili, wakati Yordani ilikuwa mara tatu au nne ya ukubwa wake. Alikuwa akimjaribu, kuona kama kweli alikuwa Yoshua.

⁷⁸ Hebu kila kitu kiende kombo. Hebu wengine wote wafanikiwe. Hebu makosa yafanikiwe. Hebu watu walio na “mfano wa utauwa, wazikane nguvu zake,” wafanikiwe, na kukusukuma nyuma. Lakini ikiwa unajua mahali unaposimama, utasimama. Haidhuru, kama ulimwengu wote ukikukataa, utasimama vivyo hivyo tu. Hutatofautiana na Neno hilo.

⁷⁹ Yordani ilikuwa mara tatu au nne ya ukubwa wake; ya kutisha, ilionekana ya kuchukiza, iliyojaa matope. Lakini Yoshua akasema, “Mungu alisema, ‘katika siku tatu,’ tutavuka. Nasi tunavuka.”

⁸⁰ Sasa makasisi wangesema, “Sasa ngoja kidogo, Yoshua. Sisi ni watu wenye elimu. Sisi ni werevu. Wengi wetu hapa ni wahandisi kutoka Misri. Tunajua jinsi ya kufanya mambo haya, kwa hivyo tutangoja tu kwa muda kidogo hata hiki kijito kitakapopungua, nasi tunaweza kuvuka. Hiyo si ni rahisi zaidi?”

“Sijali mnalowazia. Mungu alisema ‘siku tatu’ tutavuka. Nasi tunavuka. Tutavuka, katika siku tatu.”

⁸¹ Angalieni kile Yoshua alichofanya. Alitanguliza nini, makasisi? La, bwana. Aliliweka Neno mbele. Kasema, “Chukueni sanduku hilo. Nanyi makuhani wote kaeni mbali Nalo. Rudini nyuma Yake. Msijaribu kuliongoza. Acheni Hilo liwaongoze.”

⁸² Hiyo ndiyo shida siku hizi. Tunajaribu kulitangulia Neno, na kulipita, na kulifanya Neno kutoshea *hiki*, Neno kutoshea *kile*. Nawatakia heri. Tunachohitaji siku hizi, ni, kulifuata Neno.

⁸³ Neno liliwatangulia. Lilipofika Yordani, ukafunguka nao wakavuka. Kampeni yake ya kwanza, alitanguliza mambo ya kwanza. Alikuwa na sababu yake. Alikuwa na sababu, kwa sababu Mungu alikuwa amemwagiza, “Dumu pamoja na Neno. Acha Neno lifanye hivyo.” Kila kampeni, walitoka kwenda vitani, kwa sababu Mungu alikuwa amemwamuru atangulize lile sanduku.

Baada ya lile sanduku kuondoka, nini kilichofuata basi? Kuimba, wachezaji wa vyombo, kabla ya vita kutokea. Haleluya!

⁸⁴ Hilo ndilo tunalohitaji siku hizi, ni kile tulicho nacho asubuhi ya leo: waimbaji, vyombo, kucheza muziki, kushangilia. Kisha litangulize Neno, lisome Neno. Ndipo vita vitaanza. Hatuna budi kushinda, lazima tu tushinde. Dumu moja kwa moja na Hilo, shika mwelekeo Wake, nalo litakudumisha wakati wa taabu.

⁸⁵ Alikuwa na sababu nzuri ya... Sasa, kumbukeni, alipovuka, kabla ya kuvuka, alituma mpelelezi huko, wawili wao, wakaipieleleze hiyo nchi. Sasa, Musa alikuwa ametuma kikundi kizima chao, lakini wote walirudi wakiwa wamechanganyikiwa. Tazameni huduma mpya. Yeye kamwe hakufanya hivyo. Anajua ambapo mna maoni elfu moja mia tano mbalimbali, mna kuchanganyikiwa elfu moja mia tano. Lakini yeye aliwatuma wawili, akasema, “Nendeni huko. Mkaipieleleze nchi.”

⁸⁶ Sasa tunataka kufikia jambo fulani ambalo sitaki mlikose. Alisema, “Sasa, mtakapovuka...” Walivuka, wakaiteka nchi, kuona kama zile ahadi zilikuwa sahihi, waone ilikuwa ni nchi ya aina gani, na jinsi inavyowapasa kuingia. Wakavuka. Majina ya wapelelezi hayajatolewa. Lakini walipoingia nchini, walifika Yeriko, yenyewe. Basi walipofika Yeriko, ilikuwaje? Walikutana na kahaba, mwanamke mwenye sifa mbaya.

⁸⁷ Nataka kuchora picha. Labda si ya kweli, lakini nataka kueleza jambo nayo. Hatuna historia ya Rahabu. Tunajua kwamba alikuwa kahaba. Hebu tuwazie kwamba alilelewa katika nyumba ambayo ilikuwa maskini hohehahe, naye akawa mwenye sifa mbaya. Naye ni msichana mdogo, mrembo. Akaenda mitaani, apate kuwapatia riziki mama na baba yake viwete; hana njia ya kufanya kazi, ila tu kuuza maadili ya mwili wake. Lakini naweza kuwazia, wakati wote, alijua hilo ni kosa. Kulikuwa na kitu ndani yake, kilichomwambia, “Si vizuri kufanya hivyo.” Alijua haikuwa sahihi.

⁸⁸ Basi siku moja alisikia kwamba kulikuwa na Mungu aliyekuwa anatenda kazi. Moyo wake ukaanza kutetemeka. Akapata mjumbe kutoka kwa huduma hiyo kuu, ambaye alimwambia yatakayotukia. Yeye alisema nini? Sasa, Yoshua alikuwa na ishara. Yoshua alikuwa na ishara zile zile ambazo Musa alikuwa nazo, haswa. Kwa hivyo wakati yeye... Rahabu hakuomba aone ishara ya Yoshua. Alisikia tu.

⁸⁹ Mfano wa Kanisa, mfano wa Kanisa la kweli ambalo limeingizwa katika ukahaba. “Mimi ni Mmethodisti leo, Mbaptisti kesho, Mpresbiteri kesho kutwa,” aliyevutwa na kuingizwa katika ukahaba.

⁹⁰ Lakini, kwa ghafla, mhubiri mdogo anaingia mjini na kusema, “Kuna Mungu aishiye, aliyeishi jana na ni yule yule leo. Nguvu Zake zingali ni zile zile. Yeye hufanya kazi zile zile alizofanya wakati alipokuwa hapa duniani.” Mawakala Wake wako barabarani.

⁹¹ Sasa, Rahabu kahaba, anayejulikana kama kahaba, alikuwa mfano wa mwaminio siku hizi, mwaminio halisi. Hakusema, “Sasa nasikia ya kwamba—ya kwamba Yoshua anaweza kufanya ishara, kwa sababu yeye ndiye halifa wa Musa. Ningependa kuona ishara hizo. Na kama ningeweza kuona ishara hizo, basi nitaamini.” Vema, haikumbidi kabisa kuonyesha ishara

hizo, kwa sababu aliamini, hata hivyo. Yeye hakuwa Tomaso. Aliamini.

⁹² Sasa, Musa, wakati alipokuwa na ishara, alishuka na kuzifanya ishara hizo, lakini ishara siyo jambo lililowapeleka katika nchi ya ahadi. Sivyo. Hizo ishara zilikuwa ni thibitisho la lile gizo.

Naye Rahabu aliamini, bila kuona chochote. Alisema, “Sote tunatetemeka.”

Si ajabu, Nikodemo alisema, “Rabi, tunajua Wewe ni Mwalimu kutoka kwa Mungu, hakuna mtu anayeweza kufanya mambo haya isipokuwa tu Mungu alikuwa pamoja naye. Sote tunajua hilo.”

⁹³ Ulimwengu unajua hilo, leo hii. Billy Graham anapaza sauti, “Tunapaswa kurudi kwenye Pentekoste.” Baraza la Makanisa linapaza sauti, “Tunapaswa kurudi kwa manabii, kwa wanenaji kwa lugha, kwa wafasiri wa lugha, kwa uponyaji wa Kiungu, waponyaji katika makanisa yetu, kumwacha Roho wa Mungu awe huru.” Mungu anatoa wito Wake. Watu wanaogopa utauwa halisi, na kusema, “Kila kitu, mioyo yetu imeshindwa ndani yetu.”

⁹⁴ Sasa, haikumbidi kuona ishara ambayo Yoshua angeweza kufanya kwa mkono wake au kwa fimbo. Aliamini. Alisema, “Nilisikia, na ninaamini. Na sasa ninaomba rehema.” Loo, jinsi tungeweza kuweka somo papa hapa. “Ninaomba rehema, kwa ajili yangu na nyumba yangu.”

⁹⁵ Angalia yule Mrumi usiku ule, aliyevuta upanga wake, naye alikuwa akitaka kujiua, mlinzi wa jela ya Wafilipi. Paulo akasema, “Usijidhuru. Sote tuko hapa.”

Kasema, “Nifanye nini nipate kuokolewa?”

Kasema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, wewe na nyumba yako mtaokolewa.”

⁹⁶ Kwa nini? “Wewe na nyumba yako.” Bila shaka. Nyumba yako itaokolewa pamoja na wewe. Kwa nini? Ikiwa unayo imani ya kukutosha mwenyewe kuokolewa, unaweza kuwa na imani ya kutosha kwa familia yako kuokolewa. Naam. “Wewe na nyumba yako.”

⁹⁷ Mwangalie Rahabu. Rahabu alisema, “Unirehemu. Niokoe. Sitaki kufa pamoja na hawa wasioamini. Sitaki kufa kama mnyama. Ninataka kufa mikononi mwa Yehova. Ninamwamini Mungu wenu, kwa sababu Yeye ni Mungu wa Mbinguni na duniani pia. Yeye hufanya mambo yanayoonekana. Hufanya mambo halisi. Sijawahi kumwona akifanya hivyo, lakini ninaamini, hata hivyo.” Unaona? Alikuwa hajawahi kumwona Yoshua. Alisikia tu juu ya Yoshua. Hakuwa amemwona Mungu kamwe. Hakupata kuona yoyote ya kazi za Mungu. Alisikia tu. Wengine walikuwa wameiona, naye aliamini kwa kuisikia. Sasa,

alisema, “Nataka kibali kwa ajili yangu, na baba yangu, mama yangu. Wote wawili ni wazee na viwete. Nina ndugu wengine. Nataka kuwa na imani kwa ajili yao.”

⁹⁸ Ndipo yule mpelelezi, mhubiri, akasema, “Ndiyo, anakuja huku, na tutaiteka nchi. Sasa ikiwa unataka waokolewe, waingize ndani ya nyumba.” Haleluya! “Ikiwa unaamini, nenda uwachukue na uwaingize humu, kwa kuwa hatutawajibika ikiwa wako mitaani. Lakini ikiwa utawaingiza tu ndani ya nyumba, tutawajibika,” Haleluya, ambapo ile kamba ndogo nyekundu ilikuwa ining’inizwe dirishani. “Tutawajibika ikiwa utawaweka ndani ya nyumba.”

⁹⁹ Loo, ndugu, kama kuliwahi kuwa na wakati tunaopaswa kuwaingiza wapendwa wetu Nyumbani, ni leo hii, Nyumba ya Imani. Waingizeni, kwa kuwa unakuja wakati ambapo tetemeko linakuja. Ila tu, baba na mama zetu, na kaka na dada zetu, wako salama tu wakiwa ndani ya Nyumba, maana nguvu za Mungu zitaitikisa nchi tena. Ndivyo. Na ni Nyumba ya Imani tu itakayookolewa.

¹⁰⁰ “Sasa,” yeye alisema, “siwajibiki isipokuwa uwaingize ndani ya nyumba.” Naye akawafahamisha ya kwamba hawatamwangamiza yeye wala familia yake. Akasema, “Ikiwa utawaingiza ndani, watakuwa salama.” Akawashusha kutoka mahali hapo, nao wakaenda.

¹⁰¹ Kahaba huyu mkuu, Rahabu, akawa mwaminio. Nilichukua historia yake, hapa si muda mrefu uliopita. Baada ya kuzingatiwa na kuletwa katika imani, kwa sababu ya imani yake katika Mungu, aliingizwa katika imani ya Waisraeli, mwongofu. Alichumbiana na jemadari katika jeshi, wa jeshi la Israeli. Angalieni kile Mungu alimchomtondea huyo mwanamke. Na walikuwa na... Walihamia Bethlehemu, nao wakapata mtoto wa kiume; naye mwana huyu, walimwita Boazi. Kutoka kwa Boazi; alimwoa Ruthu, kutoka kwa Ruthu na Boazi akaja Yese; kutoka kwa Yese akaja Daudi; kutoka kwa Daudi akaja Yesu. Haleluya!

¹⁰² Kwa nini? “Imani huja kwa kusikia, kusikia habari za Mungu ambaye ni Mungu wa Mbinguni na duniani, na kumwamini Yeye.” Kuamini nini? Agizo ambalo Mungu alikuwa amempa mtu aliyeitwa Yoshua, akiamini agizo hilo.

¹⁰³ Yoshua alikuwa na imani katika agizo lake mwenyewe, kama vile Musa alivyokuwa na imani. Mambo yalimwendea Musa mrama, ilionekana kana kwamba alishindwa mara nyingi, lakini alipitia humo kwa ushindi kisha akafa juu ya Mwamba. Malaika wakambebea.

¹⁰⁴ Mungu, nijalie niende namna hiyo. Jalia nishikilie agizo langu mpaka, siku moja, nitakapokuwa tayari kufa, nitauona Mwamba huo mewekwa hapo karibu nami. Yoshua anatimiza

agizo lake. Ingawa alikuwa na...Mungu atalishika kwa utakatifu, kwa sababu alidumu sawa na Neno.

¹⁰⁵ Sasa, Rahabu alijua ya kwamba Yoshua alikuwa na agizo hili. Sasa usilikose. Shikilia vitu hivyo moyoni mwako. Yoshua alikuwa na agizo; Rahabu akalitambua kabla ya kuona chochote. Alijua Yoshua alikuwa na nguvu za Mungu ambazo zingeitaka ile nchi. Akaomba rehema. Mungu alimjalilia rehema. Sasa wakati Yoshua alipoingia nchini, kwa kweli, tunajua aliokolewa.

¹⁰⁶ Lakini basi agizo lingine kubwa ambalo Yoshua alikuwa nalo, lilikuwa ni kuwagawia hao watu hiyo nchi.

¹⁰⁷ Sasa kumbukeni, “Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako,” kwa hivyo alikuwa na Neno la Mungu. “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, songa tu mbele. Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe. Sitakupungukia. Unaweza kunipungukia, lakini Mimi sitakupungukia. Lakini kama ukinipungukia, neema Yangu yatosha, nitakuchukua nikurudishe tena. Endelea tu kusonga mbele. Mradi tu unadumu na Neno Langi, nitakushughulikia.”

¹⁰⁸ Sasa ilibidi aigawanye nchi, na kulikuwa na makabila kumi na mawili ya kuigawia. Sasa vipi kama angekuwa na upendeleo? Vipi kama alilipenda kabila la Gadi kuliko alivyolipenda kabila la Efraimu? Kabila la Yusufu kuliko alivyolipenda la Yuda? Lakini hakufanya hivyo. Aliigawa kulingana na Neno lililofunuliwa na Roho. Aliigawa kulingana na kabila. Pia, angalieni, alifanya hivyo kwa ufundo, kwa upambanuzi. Kwa upambanuzi wa Roho wa Mungu, alifanya hivyo.

¹⁰⁹ Kila mmoja wa mama hao wa Kiebrania, akizaa watoto hao, aliwaita jina lao. Na kila moja ya majina yao lina maana yake.

¹¹⁰ Yakobo, wakati alipozaliwa, akiwa ni pacha, alimwita “mchukua mahali pa mwingine,” *Yakobo*. Lakini alipopata nguvu zake za ushindi, na kushindana mwereka na Malaika, Mungu alibadilisha jina lake kutoka Yakobo likawa *Israeli*, “mtawala.”

¹¹¹ Jina lina uhusiano fulani na maisha yako. Wakati Petro, mvuvi, aliposhinda, kwa imani katika Yesu, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni. Lakini nitakuita *Petro*, ambalo ni ‘mwamba.’” Linakubadilisha. Jina lako lina uhusiano fulani nayo, na mahali pako maishani.

¹¹² Basi wakati jambo hili kubwa lilipofanyika, wakati kila mmoja wa mama hawa wa Kiebrania, katika utungu wa kuzaa, aliita, tuseme “Rubeni,” ambalo lilimweka mahali pake katika Palestina, hasa vile mama huyo alivyosema, na kuliita jina lake, akalitaja. Sijayaandika yote hapa. Lakini, tuseme, *Rubeni* lilimaanisha “mchungaji wa kondoo.” *Gadi* linamaanisha “mfugaji wa ng’ombe.” Na *Efraimu* lilimaanisha “mlima mahindi.”

Sasa, kwa upambanuzi wa kiroho, Yoshua, yule kiongozi mpya, kwa upambanuzi wa kiroho, alimweka kila mmoja mahali pake, akagawa hiyo nchi sawasawa kabisa.

¹¹³ Mfano mzuri sana siku hizi, wa sababu ya sisi kumhitaji Yoshua, siku hizi. Shida siku hizi, tunapoingia katika Nchi yetu ya ahadi, Gadi anataka kufuga kondoo kama Efraimu, mmoja anataka kufuga kitu kama huyo mwingine. Kila mtu anataka kuwa vile vile. Acha Mungu ampe mtu fulani karama ya uponyaji, kila mtu anataka karama ya uponyaji. Efraimu na Gadi, na hao wote wanataka kuchanganyisha, wote wanakuja na mmoja. Lakini tumegawanyika, katika mahali petu. Wote hawana karama ya hekima. Wote hawatabiri. Wote hawaneni kwa lugha. Wote sio manabii. “Lakini Mungu ameweka Kanisani, wengine wanaotabiri, wengine wanaonena kwa lugha.” Tunataka kuwafanya wote wanene kwa lugha. Mnaona jinsi mchafuko ulivyo? Basi hamwezi kufika popote. Vema, Wafilisti wangewateka, katika muda mfupi. Hakika. Lakini wakati kila mtu, kwa kiongozi, alipowateganisha kwa upambanuzi wa kiroho na kuwaweka ndani ya ule mwili, hapo walibaki hata wakawa watu walio bora sana duniani.

¹¹⁴ Mungu, tupe Yoshua. Mungu, turudishie Yoshua ambaye atashikilia lile agizo pamoja na Neno.

¹¹⁵ Hivyo ndivyo Mungu alivyomwambia. “Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, kwa kuwa utayatafakari maneno yake mchana na usiku,” kwa kuwa alikuwa na agizo mbele yake.

¹¹⁶ Sasa, Yoshua alifanyika kiongozi mkuu jinsi gani, bila kushindwa vita kamwe, isipokuwa kitu fulani kiende kombo kanisani. Wakati Akani alipochukua kabari, haikuwa sura ya Yoshua, imani ambayo ilifanya hivyo. Ilikuwa, alichukua vazi la Babeli na kabari ya dhahabu, kutoka kambini. Ndipo alipofanya hivyo, i—ilizuia vita vyote.

¹¹⁷ Kiungo kimoja kikiumia; viungo vyote vinaumia. Kile ambacho Mungu anakijia, moja ya siku hizi, ndugu, ni Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi. Anakuja kwenye Kanisa lililojazwa na Roho, ule Upendo wa Kiungu wa Mungu umeunganisha mioyo yao pamoja sana, hata watatembea kama mmoja.

¹¹⁸ Vita, katika machafuko haya yote, havina budi kushindwa. Je, Mmethodisti yu sahihi, Mbaptisti yu sahihi, Presbiteri, Mpentekoste, Mnazarayo, Pilgrim Holiness? Madhehebu mia tisa sitini na tisa mbalimbali, mbali na Buddha na hayo, na aina zingine zote. Tuko wapi? Kuna kasoro. Kuna kabari kambini mahali fulani. Yoshua akapiga kura.

¹¹⁹ Acha niseme hivi, asubuhi ya leo, kama vile Eliya juu ya Mlima Kameli. “Ikiwa Mungu ni Mungu, na ajibu kama Mungu.” Ikiwa dhehebu la Baptisti ni sahihi, hebu tuwaone wakitoa ishara za Yesu Kristo. Ikiwa Wanazarayo wako sahihi, hebu

tuwaone wakitoa ishara, wakifanya mambo aliyofanya. Ikiwa Pentekoste ni sahihi, hebu tuwaone wakifanya jambo ambalo Yeye alifanya. Ndipo tutajua.

Wanafunzi wa—wa Yoshua walisema, “Tutakufuata maadamu tunaona Mungu akifanya kazi na wewe kama alivyofanya na Musa.”

¹²⁰ Nao wanafunzi wa Yesu Kristo wanapaswa kusema jambo lilo hilo. “Tutafanya kazi na wewe tunapooni ishara za Yesu Kristo zikifanya kazi pamoja nawe. Tutafanya hivyo.” Hayo ndiyo tunayopaswa kufanya. Ndiyo kanisa linayopaswa kusema. Huo unapaswa kuwa ndio msimamo wa kanisa la Kikristo. Ndipo mngeweza kuweka katika utaratibu, karama, ishara, wafanyikazi. Ikiwa mtu mmoja ni mponyaji wa Kiungu, hiyo haihusiani na yule anayenena kwa lugha. Yeye anenaye kwa lugha hana uhusiano wowote na karama ya unabii. Mnaona? Tuna awamu tofauti za huduma hii.

¹²¹ Sasa, wakati Mungu aliponipa agizo langu. Nimeweka msingi haya yote, kurejea, kwa kusudi hili moja. “Karama na miito havina majuto.” Hakuna mtu anayeweza kujifanya chochote. Mungu hukufanya wewe kuwa kile ulicho, kwa neema Yake. Hatuna njia ya kujitengeneza. Yesu alisema, “Nani, akijisumbua anaweza kujiongezea mkono mmoja kwa kimo chake?” Ni yupi anayeweza kujifanya mkubwa au mdogo zaidi, kwa kujisumbua? Huwezi kufanya hivyo.

Wakati Mungu alipotoa lile agizo, nililihoji. Nilisema, “Sitoshelizi, au, sitoshi. Sina elimu. Siwezi kufanya mambo haya.”

¹²² Na wengi wenu ninyi watu hapa asubuhi ya leo, mngali mnaishi hapa leo. Alipotokea hapa chini mtoni, katika mfano huo wa Nguzo ya Moto, na kusimama pale na kunena. Akasema, “Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa, kama mtangulizi wa Kuja kwa Kristo mara ya kwanza, vivyo hivyo Ujumbe wako utakutangulia Kuja mara ya Pili.”

Angalieni vile imefanya. Nuru ile inayoning’inia pale, iliingia kwenye gazeti, ikaenda kote Marekani na kuingia katika mataifa mengine.

¹²³ Daktari Lee Vayle, pale, alikuwa huko Canada wakati huo. Anakumbuka wakati ilipotokea kwenye gazeti la Canada, naamini ndivyo. Sivyo, Lee Vayle? Katika gazeti la Canada, “Nuru ya ajabu yaonekana juu ya kichwa cha mhudumu wa mahali hapo wakati akibatiza.”

Watu wengi walisema, “Ni saikolojia.”

¹²⁴ Lakini siku moja Mungu aliamua kunyamazisha vinywa vya wasioamini, maana ilidumu na Neno. Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, ni ile ile tu leo, ikiliongoza Kanisa la kiroho, ndiyo iliyoliongoza la kawaida. Alionekana

tena, na wakapiga hizo picha mbele ya wakosoaji na mbele ya wachunguzi. Hii hapa inaning'inia sasa. Ukweli usioweza kukosea; ikifanya kazi zile zile, ikiwaongoza watu kiroho, kama ilivyowaongoza kimwili huko nyuma, wakidumu na Neno. Sasa yeye alisema hilo agizo lilikuwa nini. Sasa kumbukeni, Mungu kamwe hataliondokea agizo Lake.

¹²⁵ Kama...Napenda kuwachorea, au kwa namna fulani. Tatalichukua jinsi hii hapa. *Hii* hapa ishara ndogo, hilo ndilo agizo. Sasa, huu *hapa* msalaba mdogo, katika kona moja; na Biblia, katika kona hiyo nyingine; lakini maandishi yako katikati, *hapa*, hilo ndilo agizo.

Ninakuagiza mbele za Mungu na Malaika wateule, na Yesu Kristo. Hilo agizo lilikuwa, "Waombe wagonjwa."

Swali lilikuwa, "Sitoshелеzi kulitekeleza."

¹²⁶ "Kwa sababu hii ulizaliwa. Hii ndiyo sababu ya kuzaliwa kwako na maisha yako ya kipekee, kwamba unapaswa kuwaombea wagonjwa. Ikiwa utawafanya wakuamini, na uwe mwaminifu unapoomba, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako, si hata kansa." Ni wangapi wameisoma hiyo, kwa miaka yote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Liko kote ulimwenguni.

¹²⁷ Sasa, sasa nikasema, "Siwezi kulitekeleza, kwa sababu mimi sitoshi kulitekeleza. Hawataniamini. Mimi ni maskini. Sina elimu." Hiyo ilikuwa ni mimi nikihoji.

¹²⁸ Akasema, "Kama vile Musa alivyopewa ishara mbili ili kuthibitisha agizo lake, vivyo hivyo..." Si "*utapewa*." "*Umepewa* ishara mbili. Moja ya hizo itakuwa kwa mkono wako. Hiyo nyingine itakuwa wewe utajua siri yenyewe ya moyo wao, mawazo ya akili zao. Basi kwa hili wataamini, kwa ishara hizi mbili." Sasa kumbukeni. Ninii... Sikilizeni. Msikose kupata hili. Ishara siyo agizo. Ishara inaelekeza tu kwenye agizo.

¹²⁹ Unatoka hapa nje barabarani na kuona ishara, inayosema, "Maili tano kufika Jeffersonville." Hiyo siyo Jeffersonville. Hiyo ni ishara ya kukuonyesha uko kwenye barabara sahihi.

¹³⁰ Vipi kama Musa, aliposhuka kule alikuwa na ishara, kwa fimbo na kwa mkono wake; ishara hii hapa si agizo zaidi ya ilivyokuwa kwa Musa. Vipi kama Israeli wote walisema, "Aisee, ninyi Wamisri wote, ninyi Israeli wengine wote, njoni huku. Tunaye mtu anayeweza kufanya ujanja kwa mkono wake. Mnapaswa kuuona. Tunaye mtu anayeweza kuchukua fimbo na kutengeneza nyoka kwayo. Njoni, mwone"? Hiyo ilikuwa tu kibao cha kuelekeza. Hiyo haikuwa agizo. Hawakuwa wakingoja kibao cha kuelekeza. Mungu atusaidie. Walikuwa wakingoja ukombozi.

¹³¹ Nao ulimwengu huu maskini, mgonjwa, na kiwete unangojea ukombozi, huku ukiangalia kibao cha kuelekeza. Turehemu!

Kibao cha kuelekeza si kitu ila ishara ya kuthibitisha hilo agizo. Hiyo hapo huduma mpya. Ndio kwanza ifunuliwe kwangu. “Ombea wagonjwa. Wafanye watu wakuamini.” Mungu kamwe hawezi kuyaacha hayo. Hilo ndilo agizo Lake, haidhuru nini kinachoendelea, ninashindwa kiasi gani. Mimi hushindwa vibaya. Laiti nisingaliendelea mbele na ishara hizo. Hayo hayakuwa mapenzi ya Mungu, lakini Mungu ameyabariki, hata hivyo. Lakini niko tayari kuondoka kwenye mlima huu. Ninataka kuvuka Yordani, nataka kulibeba hilo agizo. “Wafanye watu wakuamini.”

Nikasema, “Hawataniamini.”

“Kutaongezewa ishara mbili.”

¹³² Sasa shida yake ni kwamba, tumekuwa tukiitazama ishara. “Loo, Ndugu Branham! Unaona? Unaweza mkono wako juu yake, wewe, loo, unapaswa kuona kile kinachofanyika. Simama mbele yake wakati upako uko juu yake, naye atakwambia kila kitu kilichoko moyoni mwako.” Hiyo ni kweli.

¹³³ Niliingia hospitalini hapa, hivi majuzi. Kulikuwa na madaktari, wasingeweza kupata tatizo la huyo mwanamke. Madaktari walipoondoka chumbani, yule mwanamke akarudi nyuma. Naye alikuwa amesimama, juu ya kitanda, na, “Walisema hawawezi kunipata na chochote, tatizo langu.” Kasema, “Ndugu Branham, unaweza kuniambia.”

Nilisema, “Ikiwa utaniamini, naweza.”

Akasema, “Naamini.”

¹³⁴ Naye Roho Mtakatifu akasema, “Tatizo *hili na lile*. Hilo ndilo. Hasa. Sasa angalieni kama silo.” Yeye ni mshiriki wa kusanyiko la Junie Cash.

Mwanamke mwingine hapo, akasema, “Mgongo wangu.” Akasema, “Hawawezi kupata nini kilichousababisha.”

Nikasema, “Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake?”

Akasema, “Naamini.”

¹³⁵ Nikasema, “Kilichotukia, nyuma huko mapema mwezi wa Juni, wewe. . . Wao—wanajaribu kukushughulikia, na kujaribu kukufanyia upasuaji wa pingili ya uti wa mgongo iliyoteleza. Sivyo. Ni mshipa uliobanwa. Uliupata kwa kuinua mzigo, wakati ulipofanya kazi na Soko la McSpaddin.”

Akasema, “Nakumbuka ilipotendeka. Nakumbuka sasa.”

¹³⁶ Hiyo haimponyi. Hiyo inaelekeza tu kwenye agizo. Acheni kuegemea kwenye kibao cha kuelekeza. Hima twendeni mjini. Hebu tuondoke kwenye mlima huu. Twendeni mjini. Hima tuvuke Yordani.

¹³⁷ Nimekosea. Nimefanya makosa. Hiyo ndiyo sababu nimewekea msingi mahubiri haya jinsi nilivyofanya. Maana, Yeye alisema, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo

nitakavyokuwa pamoja na wewe,” na hapo Mkono huo ukashuka na kuelekeza kwenye Maandiko yayo hayo. Kwa muda mrefu nimeshangaa, kwa sababu sikujua hilo agizo lilikuwa nini. Nimetafuta kitu cha kimbinguni zaidi ya hicho. Mungu hawezi kuliacha agizo Lake. Mungu alitoa hilo agizo, halina budi kubaki hivyo.

¹³⁸ Lakini Wapentekoste wote wanapenda ishara. Wanapenda kuiona. Biblia ilisema, “Kizazi kiovu na cha zinaa hutafuta ishara.” Lakini hilo agizo lilikuwa, “Ombea wagonjwa.” Na makumi ya maelfu mara maelfu, ambao nimeshindwa kuombea, kwa sababu wote walitamani ishara. Wote wanaitamani.

¹³⁹ Hivi majuzi, nilikuwa nikijaribu kufanyiza huduma, nikaingiza chumbani. Ndipo mtu akaja jukwaami, akasema, “Sasa, Ndugu Branham, ngoja kidogo. Ugonjwa wangu ni tofauti. Sina budi kujua jambo fulani.” Nikasema, “Vema, daktari angeweza kukufanyia uchunguzi.”

“Loo, sitaki hilo. Na—nataka kujua sasa hivi. Kisa changu ni tofauti sana.”

Nikasema, “Vema, nachukia kufanya hivi, ndugu.” Nikaingia ndani yake. Na muda si muda mwajua, Roho Mtakatifu akaifunua.

Akasema, “Bwana asifiwe. Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Ninyi wengine njoni sasa. Hebu niwaombee.”

¹⁴⁰ Nilipofanya hivyo, unajua huyo mwingine alivyosema? “Kisa changu ni muhimu tu kama chake.” Ndipo nikapata kama sita au nane, kisha nikafunga huo mkutano. Karibu uniue.

¹⁴¹ Daima nimeshangaa, kwa nini huo unifanye hivyo? Ni kwa sababu nilikuwa nikifanya vibaya. Hiyo ni kibao tu kinachoelekeza kwenye lile agizo. Si agizo lenyewe. Kibao hicho cha kuelekeza kimetiliwa mkazo, kote ulimwenguni. Na lugha, Afrika, India, Asia, Ulaya, kote ulimwenguni, kupitia makumi elfu na mamilioni ya watu, wanajua kuhusu kibao hicho cha kuelekeza. Niko tayari kuondoka kwenye mlima huu. Nataka kuvuka Yordani. Ninataka kuingia katika kitu kingine huko ng’ambo, ambapo imani yangu itafikia kiwango fulani, ninapowaombea watu, wataponywa.

Tazama, Mungu anairudisha moja kwa moja mkononi mwa watu wenyewe. “Ulizaliwa upate kuwaombea wagonjwa. Ikiwa unaweza kuwafanya waamini.”

Nilisema, “Hawataamini.”

¹⁴² Akasema, “Nitakupa ishara mbili, na kwa hizi wataamini.” Angalieni, basi, ishara hizi, wamekusanyika kwazo, vibao vya kuelekeza, badala ya lile agizo. “Wakiamini kwamba ulitumwa upate kuomba.”

143 Sasa wakati watu wanapoingia mstarini, kuombewa, mara tu mtu anapofika mahali hapo... Hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake mpaka wafike mahali hapo. Nao wanapopafikia, basi nasema, "Nakupa..."

144 Hattie Wright, yeye, nadhani yuko hapa asubuhi ya leo, ameketi pale pale. Alikuwa ndiye wa kwanza, tulipoona wale kuchakulo; naye alijua lile agizo kuhusu jambo hilo, na wakati mara hizo saba za moja kwa moja ambapo Mungu aliumba kitu fulani. Nilisema, "Huyo ni Mungu yeye yule ambaye angemuambia Ibrahimu kondoo dume, kumsadikisha juu ya agizo lake; ni Mungu yeye yule anayeweza kuumba kuchakulo, kwa sababu huyo ndiye niliyehitaji."

145 Maskini Hattie Wright hapo, ameketi nyuma ya hili jengo. Huku moyo wake ukiwa mbali na mambo ya ulimwengu, alikuwa akiamini. Akasema, "Ndugu Branham, hiyo si kitu ila kweli." Yeye hakusema tu kutoka *hapa*. Mungu alinena kutoka moyoni mwake.

Nikasema, "Hattie, omba utakalo. Nitakupa."

Alisema, "Je, niombe nini?"

146 Nikasema, "Una baba na mama wakongwe wameketi hapa. Una dada kiwete. Angali ameketi kwenye kiti kile. Unaweza kuomba kwa ajili yake. Unaweza kuomba kwa ajili ya mama yako, baba. Wewe ni maskini. Huna pesa zozote. Omba utakacho."

Akasema, "Vema, sijui niombe nini." Kasema, "Sijui kabisa." Akasema, "Shauku yangu kuu zaidi ni wokovu wa wavulana wangu wawili."

147 Nikasema, "Nakupa wavulana wako, katika Jina la Yesu Kristo." Nao wote wawili wameongoka, wanampenda Bwana Yesu. Wote wawili wameshabatizwa katika Jina Lake, na wanamtumikia Mungu, kila siku, kwa moyo wao wote.

Ed Daulton, ameketi hapa mahali fulani, papa hapa chini. Kuhusu watoto wake, jambo lile lile.

148 Nimeona, angalau, katika uamsho, mia nane au mia tisa, labda watu elfu moja wakipitia jukwaani, katika mkutano, mmoja mmoja. Muda si muda mwajua, ninaenda na kuwaombea. Hakika, wanapata afya. Ndipo huyu hapa msichana mdogo anakuja, akifa kwa lukemia. Hakika, nilijua tatizo la huyo mtoto. Kamwe sikusema neno kwa yeyote wao. Lakini wakati mtoto huyo alipofika hapo, nilisema, "Kipenzi, nakupa shauku ya moyo wako. Una lukemia. Nami nakupa uponyaji wako, katika Jina la Bwana Yesu."

149 Nikaligeukia kusanyiko. Nami nikasema, "Ninatoa changamoto kwa yeyote wenu hapa: Mpeleke msichana huyo kwa daktari, afanyiwe uchunguzi, muone kama ana chembe hata moja ya lukemia." Kwa nini? Mtoto huyo alikuwa amesikia,

kama vile Rahabu kahaba. Akaamini kwa moyo wake wote. Ndipo Mungu, kupitia Roho Wake, akarudi nyuma na kusema, “Huyo ndiye.” Mamia walikuwa wamepitia jukwaani, pasipo, niuavyo mimi, kupokea chochote. Niliwaombea tu.

¹⁵⁰ Moja kwa moja kuwarudia watu wenyewe, “Ikiwa utaamini.” Agizo lilitolewa. Hicho ndicho cha asili. Kibao cha kuelekeza kimetolewa. Sasa ikiwa unaweza kuamini hilo, ikiwa utaamini kwamba Mungu alinituma ulimwenguni kuwaombea wagonjwa, nitaweza kukuombea maombi ya imani. Hivyo ndivyo tu inavyoweza kufanywa.

¹⁵¹ Mungu hawezi kamwe kuliacha agizo Lake. Nimemkosea. Nimekuwa hapa, yapata miaka kumi na minne, bila chochote ila upambanuzi pekee, kote na kote ulimwenguni, mpaka makumi elfu ya nyakati, visa milioni moja, nadhani. Nawauliza jambo moja, je, uliwahi kushindwa? La, bwana. Na ikiwa kibao cha kuelekeza hakitashindwa, ni zaidi sana vipi lile agizo halishindwi kamwe. Ikiwa hiyo ishara, hiyo ni sehemu ndogo; ikiwa ishara inayoelekeza mjini, ikiwa haikosi kukuonyesha mji uko, ni zaidi sana jinsi gani huo mji utakuwapo wakati utakapokuja. Hilo hapo agizo.

¹⁵² Sasa huduma yangu inabadilika. Imebadilika tayari. Kungali kutakuwa na upambanuzi. Ungali utaendelea kadiri ninavyojisikia kwamba Mungu anataka niyaseme. Lakini hadi wakati huo, nitaomba, nitawawekea wagonjwa mikono, kama Yeye alivyoniambia nifanye, na kutekeleza agizo langu. Nimelisubiri jambo hili muda mrefu, lakini ninaamini sasa tuko tayari kuichukua ile Nchi ya ahadi. Na kwa hakika kama vile itakuwako, kutakuwa na akina Rahabu wanaosubiri, kutakuwako na mtu fulani anayengojea ambaye ataliamini kwa moyo wao wote.

¹⁵³ Je, mnaweza kuelewa? Kila mtu anaelewa hilo vizuri, inua mkono wako. Ni wangapi wanaamini kwamba hilo ni Maandiko kabisa? Ni yale aliyosema hasa. *Hili* hapa ndilo agizo; *hivi* vilikuwa vibao vya kuelekeza kwenye lile agizo.

¹⁵⁴ Sasa ninatoa changamoto kwa mtu yeyote kuniambia, mahali popote ulimwenguni, kwenye kanda hizi, popote zinapoweza kwenda, anionyeshe wakati mmoja ambapo Yeye alipata kushindwa kusema jukwaani, au huko nje katika ono lolote au chochote, ila kile kilichokuwa ni kweli kabisa, kikatimia jinsi tu Yeye alivyosema. Akamwambia kila mtu shida zao zilikuwa ni nini, na yote kuhusu hilo, na wametoka wapi, na yote kuhusu yale wanayopaswa kufanya. Na kila wakati iliposema BWANA ASEMA HIVI kwa chochote cha uponyaji, lilitokea hivyo. Ikiwa unajua moja, niarifu kulihusu. Nitaenda kwenye hiyo kanda nipate kujua. Kamwe haijawahi kushindwa, katika miaka hii mirefu kumi na miwili, au, miaka kumi na

minne. Haijawahi kushindwa, kwa sababu haiwezi kushindwa. Hiyo ishara ilitolewa na Mungu. Haiwezi kushindwa.

¹⁵⁵ Na kabla Mungu hajatoa hiyo ishara, Yeye alitoa lile agizo, kabla ya kuwepo na ishara ya kuelekeza kwenye hilo agizo. Kabla hapajakuwapo na ishara ya kuelekeza kwenye mji, inabidi pawe na mji, kwanza, wa kuelekezewa. Ikiwa umeamini kwa moyo wako wote, utapokea. “Kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule, naye Mungu atawainua.”

¹⁵⁶ Sasa, nimeegemea sana kwenye kibao cha kuelekeza, mimi mwenyewe. “Bwana, Wewe nionyeshe kuhusu hili kabla sijawaombea, maana sijui nifanyeje.” Jinsi hiyo ilikuwa kali! Ninaliomba kusanyiko linisamehe. Makusanyiko ya ulimwenguni, ambao mnaisikiliza kanda hii, samahani. Nilikuwa makosani. Kamwe sikupaswa kuliendeleza namna hiyo. Hilo halikuwa agizo Lake kwa kuanzia. Hiyo ilikuwa ishara inayoelekeza kwenye agizo. Nilipaswa kuwaombea wagonjwa, kila mahali.

¹⁵⁷ Sasa, mnaona, imerejeshwa moja kwa moja tena kwa watu wenyewe, ikiwa utaamini kuwa Mungu ameamuru jambo hili lifanyike. Hili hapa katika Neno, ni sawasawa na Neno kabisa, lile agizo. Nami nasema. . .

¹⁵⁸ Ninachora hapa kwa kidole changu, upinde, upinde wa mvua. Hilo ni agano, alilofanya Mungu pamoja na watu. Alifanya agano na jamii ya wanadamu, hatauangamiza ulimwengu tena kwa maji. Alifanya agano na kila mmoja wa mitume Wake. Alifanya agano na nabii.

¹⁵⁹ Na kule, miaka kumi na mitano, kumi na minne, kumi na mitano iliyopita, mnamo mwaka wa 1937. Tarehe 7 Mei, 1937, nadhani ndio. Ambapo, Mungu alifanya agano na mimi, akisema, “Ulizaliwa katika ulimwengu huu, kuwaombea wagonjwa. Ikiwa unaweza kuwafanya wakuamini. . .” Moyo wangu daima ulikuwa kwa ajili ya watu. “Ikiwa utafanya watu hao wakuamini, halafu uwe mwaminifu unapoomba, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako.”

¹⁶⁰ Ninasema haya kwa unyofu na kwa soni. Ikiwa kuna mtu yeyote anayepaswa kuwa na imani, itakuwa ni mimi. Kuona kile Yeye amefanya, mahali aliponitoa, shimo nilimochongewa! Kuona, kote maishani, kile amefanya! Unaona, ninaposimama na kusema jambo fulani, Mungu atakuja karibu moja kwa moja na kuliunga mkono, ukweli.

¹⁶¹ Miaka kadhaa iliyopita, wakati nilipowaambia kulikuwa na Malaika aliyenijia kichakani. Nilipokuwa na umri wa miaka mitatu tu, Nuru, upepo wa kisulisuli ukizunguka-zunguka kichakani, na kuniambia, “kamwe usivute sigara, kunywa pombe, wala chochote kile,” kungekuwa na kazi nitakayofanya nikiwa mtu mzima. Mlikuwa na haki ya kushuku hilo. Hamkuwa na haki, bali mngeweza kulishuku.

¹⁶² Huku chini mtoni, wakati Yeye aliposhuka na kujithibitisha Mwenyewe kuwa hivyo. Huko tulikokuwa tumesimama, wengi wenu mlioketi hapa asubuhi ya leo mlikuwa mmesimama pale, mkiwapo. Wengi wenu mnajua hiyo kuwa ni kweli.

¹⁶³ Wengi wenu mnakumbuka basi wakati lile agizo lilipotolewa. Ndipo Yeye akasema, “Nenda, nayo huduma hii itaenda kote ulimwenguni, uamsho utaanza.” Na kumekuwa na uamsho usiopata kutokea. Uamsho bado unaendelea, kote ulimwenguni sasa, miamsho mikubwa sana ya uponyaji ulimwenguni kote.

¹⁶⁴ Na mimi, kutoka kwa mtu, maskini haini. Sisemi hivi, sio kumwaibisha mama yangu anayeketi pale, au hayati baba yangu ambaye ametuacha, ambaye mazishi yake yalihubiriwa kwenye mimbara hii. Nililelewa katika familia mbaya sana. Mnajua hilo. Hakuna mmoja wetu Mkristo. Baba yangu alikunywa pombe. Mungu alimchukua mtoto wa mlevi, na angeniosha katika Damu Yake. Wakati ningeenda katikati ya mji kuzungumza na mtu, nami ninazungumza na mtu fulani, angeongea nami tu kwa sababu hakuna mtu mwingine wa kuzungumza naye. Mtu fulani angekaribia, tuseme mtu yeyote, haidhuru ni nani aliyekaribia, wangeniacha kwa sababu nilikuwa mtoto wa mlevi. Na wengi wenu nyinyi watu hapa kanisani mwangu mwenyewe mnajua hiyo ni kweli. Nilikuwa na jina kana kwamba sijaninii... ama kama la mnyama ama kitu fulani. Hata wakati mmoja mjini, mtu aliyekuja nyumbani kwetu aliambiwa, kasema, “Hivi ungejikusisha na takataka kama hiyo?” Loo! Bali, Mungu, ilinibidi kuendelea na nini ila Damu ya Yesu Kristo. Sina elimu. Sina utu. Sina chochote.

¹⁶⁵ Nilimwambia mke wangu, si muda mrefu uliopita, “Wazia ilivyokuwa wakati hakuna mtu angeongea nami. Nami nawapenda watu. Hawangenisikiliza.” Nakumbuka nikisoma kitabu, nikienda shuleni...

¹⁶⁶ Niliwapeleka watoto wangu shuleni, hivi majuzi. Nami ningeweza kuwanunulia vitabu na kadhalika. Na jinsi nilivyoshukuru! Ningeenda shuleni, bila viatu, nywele zikining’inia shingoni mwangu; bila nguo; nimevaa maskini koti chakavu, bila shati ndani yake. Sikuwa hata na penseli, wala kipande cha karatasi cha kuandikia. Ilinilazimu kuomba penseli, penseli ya senti moja na kipande cha karatasi, kuandika maswali yaliyokuwa ubaoni, au kitu fulani. Hakuna kitu. Nilikosea...

¹⁶⁷ Pia nakumbuka nikisoma kitabu, siku moja, ambapo Abraham Lincoln alishuka kwenye ma—mashua huko chini, naamini, New Orleans. Hapo akaona maskini watoto wadogo wa Kinegro wamesimama malishoni, kwa miguu yao midogo, ambapo ng’ombe mkongwe alikuwa amelala usiku kucha, akaondoa jalidi ardhini. Naye alikuwa...Walikuwa

wamesimama pale wakiimba, “Una viatu, nami nina viatu, na watoto wote wa Mungu wana viatu.”

¹⁶⁸ Wakati aliposhuka kwenye hiyo mashua, akaangalia. Kwenye zizi la maksai alisimama mtu mweusi mkubwa mno, mwenye afya, amesimama pale. Maskini mke wake pamoja na mtoto mchanga mikononi mwake, akilia. Walikuwa wakimpiga mnada, wakamzalishe pamoja na wanawake wakubwa zaidi, wapate watumwa wakubwa zaidi.

¹⁶⁹ Lincoln aliikunja mikono yake namna *hiyo*, akagonganisha ngumi zake. Akasema, “Hiyo ni mbaya.” Kasema, “Siku moja nitaigonga hiyo, hata ikigharimu maisha yangu.” Iliyachukua maisha yake. Lakini aliigonga, na akaiangamiza.

¹⁷⁰ Nikasema, “Ulevi huu, haya maisha mabaya, ni kosa. Siku moja nitayagonga.” Ningegongaje, nikiwa na jina kama nililokuwa nalo? Hakuna mtu angeongea nami. Hiyo ndiyo sababu nilihoji agizo langu. Hakuna mtu aliyenijali. Hakukuweco na yeyote, mahali popote; ila miongoni mwa watu wangu hapa.

¹⁷¹ Kwa neema ya Mungu, inanilazimu kuondoka nyumbani kwangu; hata siwezi kukaa mle, huku watu kote ulimwenguni, wakipiga simu. Watu wa kila namna, wakuu, watawala, wafalme, watu mashuhuri, wafanyabiashara, mawaziri, kutoka kote ulimwenguni, wakipiga simu; kupiga, kupiga, kupiga simu, siku baada ya siku, usiku baada ya usiku. Ilisababishwa na nini? Damu ya Yesu Kristo iliyo nafsini mwangu. Kama vile damu ya Abraham Lincoln ilivyofungua mkanda wa utumwa kutoka kwa mtu mweusi; Damu ya Yesu Kristo iliondoa pingua za dhambi kutoka kwangu. Na akanichukua kutoka kwenye jina ambalo lilikuwa duni kuliko jina la mnyama, na kunipa jina kama mwana wa ninii Yake—wa neema Yake.

¹⁷² Niko tayari kwenda Yordani, asubuhi ya leo. Niko tayari kulitetea agizo langu. Nimewapenda watu. Nimewahudumia. Amekutana nami, ono baada ya ono, ambayo sina wakati wa kuyaelezea, nanyi mnajua. Imeandikwa papa hapa, nyuma ya vitabu hivi, ikisema, “Unawashughulikia watu sana kupita kiasi. Kutembea na Mimi, utatembea peke yako. Unaweka mkazo sana juu ya ishara hizo.”

¹⁷³ Sikujua mengine yalikuwa ni nini, lakini saa imewadia. Saa imewadia, wakati nilipoona Mkono ukishuka juu ya Yoshua, kasema, “Nilikuwa pamoja na Musa. Nitakuwa pamoja na wewe.” Ninaliamini, asubuhi ya leo. Tangu sasa, na leo hii kuendelea, nitamtumikia Mungu katika agizo langu. Ikiwa anataka kunionyesha ishara, au anataka kunionyesha maono, anaweza kunionyesha. Asiponionyesha; kamwe sitasimama mbele ya watu, nikijaribu kuiacha imani yao ivute kitu kutoka kwangu, tena. Nitawaombea wagonjwa na kuwakabidhi kwa Mungu, na kuwaacha waondoke. Ikiwa wanaamini lile agizo,

Mungu ni mkweli vile vile. Amenileta umbali huu, kama vile tu alivyomfanyia Musa. Kama vile tu alivyomfanyia Yoshua, amefanya vile vile.

¹⁷⁴ Ombi langu nyenyekevu ni, “Mungu, nisamehe. Jalia niamke na kujaribu tena. Nisaidie, Bwana. Jalia niwaongoze watu hawa, na kuwaweka kwenye Neno, tupate kwenda hadi Yordani, tuingie kwenye Nchi ya ahadi, ambako Kanisa kubwa la Mungu lililokombolewa litaokolewa lisitende dhambi tena.” Hiyo ndiyo shauku yangu asubuhi ya leo. Amini, ukaishi. Amini, na uponywe. Ninazungumza nanyi katika Jina la Bwana.

Na tuombe.

¹⁷⁵ Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, na Mpaji wa kila kipawa chema, jalia rehema na neema Yako ziwe juu ya mtumishi Wako, kwanza, Bwana. Nimekosea machoni Pako, kwa kutumia vibaya kitu ambacho kimekuwa cha Kiungu, kwa sababu watu wamekivuta kutoka kwangu, Bwana. Ninakuomba, Ee Bwana Mungu, tangu saa hii na kuendelea, uniagize, Bwana, kwa Roho Wako. Ninaamini, kwa moyo wangu wote. Wewe, saidia, kutokuamini kwangu.

¹⁷⁶ Na wakati wanaume na wanawake wanapokuja kuombewa, hayo nitafanya maadamu utanipa pumzi na uhai. Jalia sasa waamini, wakati wakiombewa, Baba. Jalia agizo hili ambalo Wewe umenipa, jalia niweze kulipeleka kote ulimwenguni. Ndipo ninapofika mahali fulani ambapo ubao wa kuelekeza umepigiliwa, jalia wajue kwamba huo unaelekeza tu kwenye lile agizo. Jalia wawe na imani.

¹⁷⁷ Bwana, sitangojea tena a—aina fulani ya ishara au kitu fulani kuniambia mambo fulani, ama kama mtu *huyu* atapona. Nitaenda kukutana na adui, nikiwa na imani moyoni mwangu. Nitaenda kumpa changamoto, dhidi ya Damu ya Yesu Kristo, kwamba kwa Damu ya Kristo, hawezi kusimama.

¹⁷⁸ Sasa, ikiwa mambo haya yote yamekuwa sawa, ambayo yamethibitishwa kuwa ni kweli, basi Wewe utawaponya wagonjwa ninapowaombea, Bwana. Ni Neno Lako. Ni ahadi Yako. Hili ninatamani kufanya. Wewe, saidia, kutokuamini kwangu.

¹⁷⁹ Samehe dhambi zangu, Bwana, za kukuasi. Sikujua nifanye nini tena. Mimi, kama nilifanya, Bwana, halikuwa limefunuliwa na kufanywa dhahiri kwangu. Sasa ni dhahiri. Najua ninakosimama. Najua agizo langu. Nami kamwe sitaruhusu Neno hili liondoke kinywani mwangu, mchana wala usiku. Sikuzote nimelitetea, Bwana, nikalitetea, nikiwaambia watu. Kwamba, iwapo si Neno la Mungu, ninalishuku. Bali ningehubiri ama nisifanye kitu isipokuwa kiwe ni Neno la Mungu.

¹⁸⁰ Lakini Bwana, ninachoka, nikikanyaga-kanyaga eneo lili hili. Kama nilivyosema jana usiku, “Miaka arobaini jangwani,

huku na huku, huku na huku.” Mungu akibariki, naam, kufuga kondoo na watoto, na yoyote yale, na makundi ya mbuzi na ng’ombe, na yote hayo. Mungu, Wewe uliwabariki. Lakini siku moja ukasema, “Mmekuwa kwenye mlima huu muda mrefu kutosha. Loo, pandeni kaskazini, kuelekea Yordani.”

¹⁸¹ Mungu, ninaanza, asubuhi ya leo. Ninaacha vibao hivi vya kuelekeza, kwa sababu vinaelekeza kwenye Nchi bora. Naweza kujikwaa. Huenda nikapitia kwenye Waamaleki. Huenda nikapitia kwenye Wahiti, kwenye Wakanani. Huenda nikalazimika kupitia ukosoaji wangu mwenyewe. Bwana, nitaendelea tu kusonga mbele. Ninajua kuna Nchi kule, mahali fulani. Kuna mahali fulani, hali fulani, mahali fulani tunapoweza kufikia, ambapo Wewe utayajibu maombi, kwamba chochote tuombacho tutapewa; hata kansa haitasimama mbele ya maombi. Najua huo ni ukweli. Kwamba ninaamini, na ninangojea, Bwana ninapojikabidhi Kwako, asubuhi ya leo, kwa ajili ya utumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Amini tu, amini tu,
Yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yawezekana, amini tu.

¹⁸² [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Sasa, kanda ilizimwa, kwa sababu huu utaenea ulimwenguni kote. Hiyo ni kutoka moyoni mwangu. Je, mnaweza kuelewa, kanisa?

¹⁸³ Mungu kamwe hawezi kusema chochote na kukighairi. Maneno Yake hayakosei. Ahadi Zake ni za kweli. Wakati huu wote, nimekuwa nikingojea saa hii. Mnaona? “Maombi ya imani ndiyo yanayowaokoa wagonjwa,” si ishara. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Ikiwa unaweza kuamini,” Yesu alisema, “Naweza. Ninaweza, ikiwa unaamini.” Sasa ikiwa Mungu amenipa nguvu za kuomba maombi ya imani juu yako, na ameiahidi na kuthibitisha kwamba ni kweli, sasa mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Ninachoomba, ninapokea, ikiwa unaamini. “Kama unaweza kuwafanya watu waamini, na uwe mwaminifu uombapo, hakuna kitu kitakachosimama mbele ya maombi yako.”

¹⁸⁴ Ndugu, dada, endapo kwa vyovyote nilitaka kuwa mwaminifu, ni sasa, baada ya makosa yangu yote kuonekana. Ninachotaka... Sababu ya kuzileta Jumbe hizi, hapo awali, kwamba Mungu huonyesha pale kwamba Yeye ni mwenye rehema. Musa alifanya makosa yake, mtu mashuhuri kama yeye. Kisha Yoshua alipojitokeza, alikuwa akienda kufanya yake, pia. Lakini Mungu alisema, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.”

¹⁸⁵ Sasa mwangalie Mungu, miaka miwili iliyopita, akielekeza Andiko hilo moja kwa moja kwangu. “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.

Sitaangalia makosa yako.” Alijua kuwa saa hii ilikuwa inakuja. Sasa iko hapa, mnaona, imerudi moja kwa moja tena, maana Mungu hawezi kamwe kuiondokea.

¹⁸⁶ “Kwa imani umeokolewa.” Ni wangapi wanaojua hayo? Sio wengi, ni watu wangapi wazuri wanaokuombea, ni wahubiri wangapi wazuri wanaokuhubiria, lazima uwe na imani yako binafsi kwa ajili ya wokovu. Hiyo ni kweli? Ni yako mwenyewe. Sijali unasikia mahubiri mangapi mazuri, wewe ni mfuasi wa makanisa mangapi mazuri, ni imani yako binafsi inayokuokoa. Unalia kwa sauti kubwa jinsi gani, unasihi kiasi gani, unapiga kelele kiasi gani, unacheza kiasi gani katika Roho; unaokolewa tu kwa imani yako. Hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo njia pekee ya kuponywa.

¹⁸⁷ Kama Mungu akimpa mtu ujumbe, mhubiri; mhubiri anahubiri wokovu na anatoa ujumbe, unaona ujumbe huo ni wa Kweli, Mungu anauthibitisha kwa Neno Lake, kwamba ni Kweli. Basi ni zaidi sana vipi unapaswa kuamini karama ya uponyaji, wakati imethibitishwa na Neno na Malaika. Kwa ishara mbili ambazo zimeonyesha kutokukosea kwa zote mbili, ni zaidi sana vipi unapaswa, unaamini! Unaona? Na mradi...

¹⁸⁸ Kuonyesha kwamba haikuwa ni mapenzi makamilifu ya Mungu hasa kufanya hivyo, ishara hiyo sikuzote ilinidhoofisha. Ni wangapi wanaojua hayo? Muulize mke wangu huko nyuma, anaweza kukwambia. Huyu, anateseka vibaya kuliko kila mtu; inambidi kunivumilia. Ni vigumu kujua mahali ulipo, na kutembea-tembea, na—na *hili, lile*. Hujui tu, u—unashuka barabarani kidogo, kisha unasimama.

¹⁸⁹ Sasa, nikitoka kwenye mikutano hii ya mwisho. Niliwachukua hao watu mstarini. Kwanza, tungekuwa na usiku kadhaa, tatu, bila kusambaza kadi za maombi. Ndipo unapata kusanyiko kubwa sana, ingetubidi kusambaza kadi za maombi. Ningesimama, wakati mwingine, na kuwapitisha hamsini au sabini na watano. Labda niwe na upambanuzi arobaini au hamsini, kwa wakati mmoja, katika kila usiku. Hiyo ni kweli, Gene, Leo, nanyi mlio karibu na hapa, mlio mkutanoni? Hakika ilikuwa kweli! Nayo ilifanya nini? Wakati iliponiacha, kuanza kwenda nyumbani, ningesahau mahali nilipokuwa; nataka kujua nilikotoka, kwenye barabara kuu.

¹⁹⁰ Basi unataka kuniambia, Mungu humfanyia mtu hivyo? La, bwana. Ilikuwa ni mtu akijifanyia mwenyewe, kwa kuchukua kibao cha kuelekeza badala ya lile agizo. Nilisimama chini ya maskini mti wa siku nyingi huko, kando ya barabara, mahali fulani huko Washington, au mahali fulani huko juu. Nikasema, “Bwana, laiti ungeniruhusu tu nijitikise nipate kujirudia, vizuri tena, unisaidie kujua yaliyo kweli, kusudi niweze kujinyosha mara moja pamoja na watu, na kuliweka agizo sawasawa.”

¹⁹¹ Ninalo sasa. Nikiketi hapa chini kando ya mlima, wa Kentucky, hivi majuzi, kwenye mapambazuko asubuhi moja, Yeye akanifunulia. Nalo ndilo hili; ndilo hili. Sasa naenda katika Jina la Bwana Yesu. Uh-huh.

¹⁹² Liaminini, mpate kuishi. Liaminini, mpate kupona. Siwezi kumfanya mtu yeyote kuliadini. Inakubidi kuliadini, wewe mwenyewe. Lakini nimewaambia Kweli. Mungu ameshuhudia kwamba ilikuwa Kweli, kwa Neno Lake, kwa Malaika Wake, kwa ishara na maajabu, kwa miaka mirefu kumi na miwili. Ikiwa hawataliadini sasa, hawataliadini kamwe. Hiyo ni kweli? Lakini saa imewadia, wakati nimechoka kukaa kwenye mlima huu. Nataka kwenda hadi Yordani. Nataka kuingia katika ahadi kamili. Ninataka kupata imani ndani yangu mwenyewe, sio kuitazama ishara, sio kutazama kitu ambacho Mungu amefunua, au namna fulani ya kibao cha kuelekeza. Ninataka kuangalia kuelekea Kalvari, niseme, “Kwa imani naja, Bwana Mungu. Naja katika Jina la Bwana Yesu.”

¹⁹³ Sasa wapo wengine hapa ndani wa kuombewa, asubuhi ya leo. Naja kukabili na ugonjwa na mateso ya mwili wako, katika Jina la Yesu Kristo. Nitafanya hivyo mpaka Mungu atakapoyachukua maisha yangu kutoka kwangu. Hakika. Mradi tu ananipa akili na ufahamu, nitakuja kuomba. Usishindwe, kwa kile unachoamini, kwamba nitakapokuomba, utapona. Amua hilo. Ikiwa hauamini, basi usije kabisa, maana utajidhuru tu.

¹⁹⁴ Sasa liko kwenye kanda, na liko hapa. Tangu sasa, hakuna upambanuzi tena hadi Mungu atakaponipa ninii... atakaponiambia nifanye jambo fulani. Aseme, “Nenda, kamwambie mtu *huyu* jambo fulani,” ndipo nitakwenda kuwaambia. Yeye angesema, “Fanya jambo *fulani*,” nitaenda kulifanya.

¹⁹⁵ Lakini kuhusu kusimama pale, nikisema, “Sasa niangalie. Unaamini kwa moyo wako wote. Naam. *Huyu, fulani-wa-fulani*. Wewe ni *John Doe*, umetoka *ninii*. Ulikuwa na kansa, kwa muda *fulani*. Daktari *Nanii* alikuambia hutapata afya. Ukaenda na kufanya jambo *fulani*. Sasa huna budi kurudisha *kile*, na kusahihisha *hili*. Na kuchukua *hiki*, kabla hujapata afya. Vema. Ndugu *Doe*, nenda zako sasa, amini. Sasa, wewe ni Dada *Nanii*. Unatoka *ninii*. Unatoka *ninii*.” Huko nikaingia kwenye kimbunga, bila kujua la kufanya, ni ngumu. Ndipo muda si muda, mwajua, basi huyu hapa mwingine. Ninaangalia, na kumwona ninayemtazama. Kisha ninatoka mkutanoni, na, “Kwani niko wapi?” Hayo hayapo tena.

¹⁹⁶ Naja katika Jina la Bwana Yesu, kama mtumishi Wake. Ikiwa Mungu hajakuthibitishia kufikia wakati huu, kwamba nimewaambia Kweli, basi kamwe hutaamini nimewaambia Kweli. Amina. Hiyo ni sawa. Ni kweli. Ni wangapi wanataka kuombewa? Inua mkono wako. Sawa.

¹⁹⁷ Sasa ninamtaka Teddy. Je, Teddy bado yuko humu jengoni? [Mtu fulani anasema, “Hapana. Ilimbidi kuondoka.”—Mh.] Ilimbidi aondoke. Ni nani mpiga piano hapa, ambaye angeweza kupiga wimbo, *Amini Tu*, kwa ajili yangu, tafadhalini? Ikiwa kuna mtu hapa ambaye anaweza kucheza. Mnaye? Au, mna kanda, sivyoyote, mahali fulani? Ikiwa mtu yeyote yuko hapa ambaye anataka kutupigia, *Amini Tu*, mpiga piano, njoo moja kwa moja. Mwanamume au mwanamke, haijalishi, tungefurahi kuwa na wewe. Vema. Sasa wakati unapoucheza kwa upole, tafadhali, dada, mpendwa.

¹⁹⁸ Sasa hatutasambaza kadi za maombi. Tunapokuwa kwenye mikutano midogo kama huu, hatuzihitaji. Tunapokuwa kwenye mikutano mikubwa, bado tutalazimika kusambaza kadi za maombi, ikiwa nitawaombea mia tano. Ungali ungelazimika, kwa sababu unapata wengi sana katika ninii, wamelundikana kwenye umati, unaona.

¹⁹⁹ Ni wangapi wanaoamini kwamba haya ni mapenzi ya Mungu? Loo, kitu Fulani kinanifanya tu nihisi nimefanya vizuri. Kitu Fulani kinafanya... Limeondoka kifuani mwangu. Limeendelea kwa miaka kumi na miwili, nikijua kumekuwa na kasoro, Ndugu Lee. Sasa ninajua limeondoka hapo. Nimelisema; limerekodiwa. Nalo limeondoka kifuani mwangu sasa.

²⁰⁰ Kumbuka, unaweza kuokolewa tu kwa imani yako binafsi. Unaweza tu kuponywa kwa imani yako binafsi. Mnaamini hii ni Biblia? Neno la Mungu. Je, mnamwamini mchungaji wenu kuwa ni mtu wa Mungu, kanisa lolote unalohudhuria? Ikiwa huamini, unapaswa kuliacha. Mwendee mtu ambaye ni mtu wa Mungu. Ndipo ikiwa unamwamini, unaamini anakwambia Ukweli, basi ukubali. Imani yako binafsi katika Kristo inakuokoa. Haijalishi mchungaji wako ni mzuri jinsi gani; jinsi mama yako alivyo mtauwa, mtakatifu; jinsi—jinsi Neno la Mungu lilivyo halisi; ni kiasi gani unalia; unaomba kiasi gani. Imani yako ndiyo inayokuokoa. Kwa imani umeokolewa.

²⁰¹ Sasa jambo lilo hilo linatumika. Haijalishi jinsi gani... Neno la Mungu linasema kwamba atatuma hii katika siku za mwisho. Mahubiri mawili ya moja kwa moja sasa, nilileta Israeli wa kawaida na Israeli wa kiroho, pamoja. Tunamtafuta Yohana wa siku hizi, ambaye ni Roho Mtakatifu, atuongoze kwenye ile Nchi. Hana budi kuzungumza kupitia kwa mtu fulani, kwa sababu Yeye ni Roho. Nimewaambia kile alichoniambia. Sasa aminini, mpate kuponywa.

²⁰² Sasa hebu hawa, upande *huu* wa mstari. Doc, washuke kule. Billy Paul, Billy yuko wapi? Njoo hapa ukamsaidie, Doc, tafadhali.

²⁰³ Na sasa kila mmoja wenu anayepitia kwenye mstari huu wa maombi, kumbukeni, itawarudia moja kwa moja, ikiwa huamini kwa moyo wako wote. Ni Kweli; lazima uiamini. Sasa kumbuka,

ni wewe, ndiwe uliye mgonjwa. Mungu alilisema katika Biblia Yake. Mungu alilituma kwa mjumbe Wake. Mungu alilithibitisha kwa Malaika Wake. Sasa huna budi kuliadini.

²⁰⁴ Sasa, kwenu ninyi mnaotaka kuombewa, haya ndiyo Biblia iliyosema: “Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Na hiyo ni Kweli. Nasi tunataka kuamini jambo hilo, kwa moyo wetu wote, sasa, naye Mungu atawapa uponyaji.

²⁰⁵ Sasa njoni huku *hivi*, kupitia papa *hapa*, kisha mrudi moja kwa moja. Hebu upande *huu*, halafu upande *huu* mwingine. Rudini moja kwa moja vivyo hivyo. Hebu upande *huo* usimame upande wa kulia, *hapa*. Unasemaje? [Mtu fulani anaongea na Ndugu Branham—Mh.] Nitashuka chini papa hapa. Naam, bwana. Papa hapa chini, kuwaomba.

²⁰⁶ Sasa, hizi barua na lesu, nimeziomba. Wengi wenu, baadhi yenu, labda, inawabidi kwenda. Msisahau usiku wa leo, sasa, ibada iko juu ya thibitisho, *Thibitisho La Kiungu La Kanisa La Kweli*. Mnaona?

²⁰⁷ Sasa, kwenu ninyi mtakaoninii... mtakaoombewa, hivi mnaamini kweli kabisa mtaponywa? Ikiwa huamini, usije. Kama unaamini, ni jukumu lako kuja.

²⁰⁸ Sasa, mimi si mponyaji, lakini nina karama ya uponyaji. Hiyo ilishuhudiwa. Imethibitishwa kwamba hiyo ni kweli. Mnaona? Huko nyuma kabisa, muda mrefu uliopita, nakumbuka, nilikuwa nikienda hospitalini hapa nilipokuwa tu mhubiri wa Kibaptisti huku, mahali hapa. Ningetoka kwenda hospitalini. Kulikuwa na muuguzi mkongwe huko. Aliishi huko chini Howard Park. Sijui kama angali yuko, au la, hospitalini. Alizoea kumwambia mgonjwa, “Sasa utapona. Sasa utapona.” Kasema, “Maskini yule mhubiri wa Kibaptisti anakuja kukuomba.” Mnaona? Ilikuwa tu... Ilikuwa mwanzoni. Ilikuwa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Na sasa ilikuwa itaenea, kutoka hapa, kuuzunguka ulimwengu.

²⁰⁹ Na sasa Yeye alinipa ishara hizi, kufidia elimu yangu. Sasa kama ningalikuwa na elimu ya baadhi ya hawa wahudumu wengine, kwa mfano, mmoja ninayemjua, labda ya Ndugu Neville au Daktari Vayle, baadhi yao, i—isingenilazimu kuwa na hii. Lakini inanibidi kuwa nayo, ili kutimiza hili, kuchukua kile ambacho sikuwa nacho katika njia ya elimu. Ilibidi niwe na ishara. Na kama vile tu... Ishara zimethibitika kuwa na matokeo mazuri kama vile elimu ingefanya. Lakini, mnaona, iwapo huna sifa, Mungu anaweza kukupa sifa hiyo kwa njia nyingine.

²¹⁰ Sasa mnayo imani na mnaamini. Sasa ninataka kila mmoja wenu amwahidi Mungu, mahali unaposimama. Kwa sababu, ikiwa hutafanya hivyo, haitakusaidia. Nataka kila mmoja wenu aweke kando kila kivuli cha shaka. Na wakati ukipitia mstarini, nitakapokuomba, nataka utoke hapa. Inawezekana usione

alama moja ya matokeo. Lakini, hiyo, Yesu kamwe hakusema, “Je, uliuona? Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini? Uliamini? Kama unaamini.”

²¹¹ Sasa, nimeona jambo hili, njiani. Ninawaombea watu. Baadhi yao Yeye asingeweza; alifanya upambanuzi huo; wangeenda zao, wakisema, “Huh! Sikupata chochote. Hakuniambia chochote.” Mtu huyo kwa kawaida hakupata chochote, pia.

²¹² Lakini wengine wao walipitia mstarini, wakisema, “Asante, Bwana. Ninaamini.” Hao ndio niliosikia kutoka kwao, “Unajua, Ndugu Branham, sikusikia tofauti yoyote, kwa siku kadhaa,” labda wiki mbili au tatu, au chochote zaidi. “Lakini, mara moja, nilianza kuhisi kitu hicho kikiniacha. Unaona? Hicho, hicho hapo kikaondoka.” Mnaona? Mnaona? Mnaona?

²¹³ Unaweza kusema unaamini. Kuna matabaka matatu ya watu wanaohudhuria mkutano huu, hayo ni: wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waaminio. Baadhi yao hujifanya kana kwamba wanaamini, “Loo, naam, naamini,” lakini hawaamini. Kama unaliamini. . .

²¹⁴ Nataka kuwaulizeni swali hili sasa. Ikiwa unaliamini, haiwezekani kwako usiponywe. Sikizeni. Hebu nirudie hilo. Haiwezekani kabisa kwako usiponywe, kama unaliamini.

²¹⁵ Kwanza, Neno la Mungu lilida-. . . lilitoa agizo. Mnaamini hilo? Neno la Mungu lilisema hivyo, kwanza. Hiyo ni juu ya kila kitu. Jambo la pili, Malaika wa Bwana amethibitisha hilo, ishara zimelithibitisha. Hiyo ni kweli? Sasa, hakuna kushindwa hata mara moja, mahali popote.

²¹⁶ Hakuna kosa hata moja katika Neno la Mungu, lililosema, “Mimi—mimi wakati mmoja niliwapa uponyaji, lakini sasa ninauondoa kwao.” Nataka mtu anionyeshe hilo. Nitakuonyesha ambapo Yesu aliliagiza Kanisa Lake liwaombee wagonjwa, na maombi ya imani yatawaokoa wagonjwa hao. Sasa niambie ni wapi alisema haitatendeka tena. Nionyeshe katika Biblia. Unaona?

²¹⁷ Alisema, katika siku za mwisho atafanya mambo fulani haya, atayainua mambo haya. Angalia kilichotokea. Amelitimiza Neno Lake. Niliwaambia kwamba aliniagiza, sasa ulimwengu unajua hilo. Sayansi inajua hilo. Malaika wa Bwana analithibitisha. Na matokeo yamethibitisha kwamba ni kweli.

Tunaishi katika ulimwengu mgonjwa. Kuna mengi ya kuombea. Nilifikiri, “Hakika kuna njia nyingine, kando yake.”

²¹⁸ Ndugu Moore aliniambia wakati mmoja. . . Kulikuwa na maskini msichana mdogo akitambaa kupitia jengoni, kiwete. Maskini mtoto huyo, akijaribu kupanda mahali nilipokuwa. Nikaangalia chini. Huyo mtoto akaanza kulia. Vema, wasingemleta mstarini. Hakuwa na kadi ya maombi.

Bila kujua, huo ulikuwa ndio usiku wa mwisho wa mtoto huyo. Ndugu Moore na hao wengine walimsaidia kutoka mstarini.

Kesho yake, tuliketi na kulizungumzia. Akasema, “Ndugu Branham, hilo liliniumiza.”

Nikasema, “Ati lilikumiza? Unafikiri lilinifanyia nini mimi?” Unaona?

²¹⁹ Maskini msichana mdogo, kiwete! Hilo halikunitoka. Na hiyo imekuwa karibu miaka kumi iliyopita, maskini msichana mdogo, kiwete huko Illinois. Mwenye nywele nyeusi, macho ya kahawia, anatambaa, polio kidogo, akijaribu kufika mahali nilipokuwa. Nao mabawabu kule chini ilibidi wamsaidie na kumrudisha kitini mwake. Alitambaa kutoka kwenye kiti chake, kupanda pale. Kwa nini? Unaweza kuchukua tu idadi fulani. Na kama ningeliondosha baadhi yao, nimweke mle pasipo na kadi ya maombi, wengine wangeudhika. Mnaona? Kweli. Nisingefanya hivyo. Nikasema, “Hakika kuna njia nyingine.” Laiti ningalikuwa ninajua wakati huo ninayojua sasa, mambo yangukuwa tofauti, hakika yangukuwa tofauti.

Sasa, kila mmoja wenu, kitu pekee kitakachowazuia kupona, ni wewe kutokuliamini.

Sasa hebu tuinamishe kichwa chetu.

²²⁰ Baba yetu wa Mbinguni, hapa wamesimama vipofu, vilema, wanaoteseka, wagonjwa, wanaokufa kwa kansa, vidonda, vivimbe. Wote wamesimama hapa mstarini, Bwana. Nimelihubiri Neno. Na kwa muda wa miaka kumi na miwili, Wewe umethibitisha Hilo kote ulimwenguni. Nimeomba msamaha, nami ninajua kwamba sikufanya hivyo makusudi. Nilifanya hivyo kwa sababu nilifikiri nilikuwa nikifanya vema. Sasa naja, Bwana, naja Kwako, kwa unyenyekevu. Nikikuomba uyabariki maombi yangu, kwamba, ninapowaombea watu hawa, kila mmoja wao ataponywa. Ibariki imani yao. Saidia kutokuamini kwetu, Bwana.

²²¹ Pia jalia kila mmoja, asubuhi ya leo, kweli ashike lile ono. Jalia wasipoteze chochote chake. Lakini jalia walione, Kimaandiko, na wafikirie juu ya Malaika wa Bwana huko nyuma mwanzoni, alisema, “Kama Musa alivyopewa karama mbili.” Halafu, miaka miwili iliyopita, akileta Biblia, huku Mkono ukishuka, ambao, kama ulioandika ukutani huko Babeli; mkono wa kibinadamu, ulivyoonekana, ambao ulielekezwa chini kwenye Biblia, kwenye mlango uu huu, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.” Na, Baba, hili hapa asubuhi ya leo, limeletwa kwenye nuru. Tunakushukuru kwa ajili ya hili, Bwana. Nisamehe kosa langu.

²²² Na sasa tunapoingia kwenye mkutano huu wa maombi, jalia nguvu za Mungu ziponye kila mgonjwa anayepitia mstarini. Ninaenda tu kama mtumishi Wako, pasipo kuomba upako wowote maalum, chochote maalum. Lakini nikijua hili, kwamba

katika maisha yangu liko agizo lile, naenda kulitekeleza, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²²³ Sasa, Ndugu Neville, naomba usimame hapa. Sasa, nikiwa na karama hii, sitawapaka mafuta. Mnaona? Nitafanya tu kile Yeye alichoniambia nifanye, kama lile agizo lilivyosema, “Wafanye watu wakuamini. Kuwa mwaminifu.” Mnaamini? Basi mimi ni mwaminifu. Kitu fulani hakina budi kutendeka.

²²⁴ Ndugu Neville ataongoza katika nyimbo. Ninyi nyote ombeni, kwa utulivu, wakati nikiwaombea wagonjwa.

Bwana Yesu, ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu aliye na mawe haya ya figo. Nami nayakemea, katika Jina la Yesu Kristo. Naomba aende akaponywe.

Nini kilitukia? Shida yako?

Bwana, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu, tatizo hili la tezi dume. Na ninakemea nguvu hizi za ibilisi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Tabia hii ya tamaa mbaya...?...

Bwana, naiweka mikono yangu juu ya dada yangu aliye na miguu hii mibaya ambayo imevimba. Ninakemea uvimbe huo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nenda, amini, Dada, kama tu vile tulivyosema.

Bwana! Pamoja na matatizo ya moyo na magonjwa mengine. Ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, na kuukemea huu, katika Jina la Yesu, kwa agizo langu.

Bwana, macho yanayofifia, na tatizo la moyo. Ninaukemea, kwa ajili ya mwanamke huyu, kwa agizo langu kutoka kwa Mungu. Katika Jina la Yesu. Amina.

Haina budi kuwa. Itakuwa sawa, Dada...?...Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²²⁵ Hiyo ni kweli. Ikiwa ni wakati wako wa kwenda, huna budi kwenda kwa namna fulani. Hiyo ni kweli. Lakini, kwanza, kabla hajakwambia, ikiwa utakuwa mwaminifu na usitie shaka, utapona. Hiyo ni kweli kabisa.

²²⁶ Lazaro alifufuliwa kutoka kwa wafu. Alikufa tena. Lakini alifufuliwa kutoka kwa wafu, kuonyesha kwamba Mungu huwatimizia watu ahadi Yake. Alisema, “Mariamu, unaamini haya? Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. Nimeagizwa na Mungu, kuwafufua wafu. Unaamini hili?”

Akasema, “Ndiyo, Bwana. Ninaamini kuwa Wewe ni Mwana wa Mungu, uliyekuja ulimwenguni.”

Kasema, “Mlimzika wapi?” Uh-huh.

Ilimbidi kufa tena. Lakini alimfufua, kuonyesha kwamba Yeye ndiye Ufufuo na Uzima. Mnaona?

227 Mungu hufanya mambo hayo, na kila kitu kiko katika mpangilio wa Kiungu. Loo, ninafurahi sana kusema hivyo. Kila kitu kiko sawasawa kabisa. Ikiwa unaweza kuamini, kila kitu unachoomba umepewa. Haina budi kuwa hivyo. Vema.

Endeleeni tu kuomba sasa, wakati tunapomaliza huu mstari.

Mungu awabariki.

228 Bwana Yesu, dada yetu ni mgonjwa sana, akinisikia nikisimama hapa, nikihubiri maneno hayo. Naomba—naomba uvivu huu mdogo wa mashaka uwaondokee wote, Bwana. Jalia waamke, waondoke kwenye mlima huu wa kale wa kwenda huku na huku; wapige hatua mpaka Yordani, Bwana. Lijalie, Bwana. Naomba dada yetu apitie njia hii sasa, tangu saa hii na kuendelea, akiamini kwamba Mungu ameuponya mwili wake. Katika Jina la Yesu. Nenda zako, ukishangilia.

Mungu akubariki.

229 Bwana Yesu, mpe shauku ya moyo wake, kwa ajili ya binti yake na familia yake. Ninaomba, kwamba, katika Jina la Yesu, aupokee huu; ninapotoa maombi yangu na imani yangu, kwa kumwekea mikono. Kama sikukuamini Wewe, nisingeweka mikono yangu juu yake. Kama niliamini Wewe hutafanya hivyo, nisingemwombea. Lakini ninaamini, Bwana. Naye anaamini, pia. Nasi tunaweka imani yetu pamoja, tukiamini tunaipokea. Amina.

[Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]
Mungu, akubariki, Pat.

230 Bwana, kwa ajili ya watoto wake wa thamani anaotaka waokolewe. Una shida ya kusikia. Daktari anasema mtoto wa jicho anatokeza kwenye jicho. Anataka kuishi kwa utukufu wa Mungu. Mjalie, Bwana, ninapoomba maombi haya kwa ajili ya ndugu yangu, ninaliombea, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, ndugu. Usiwe na shaka. Amini kabisa uliloomba.

[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]
Mungu akubariki, Dada.

231 Bwana, maskini mama huyu anayesimama hapa kwa ajili ya mwanawe, ajali ya motokaa au kitu fulani, Bwana, ambacho kimemwumiza. Naye anakwenda kupandikizwa ngozi. Anaombea mwili na wokovu wake. Anawaombea wapendwa wake. Ameomba kwa ajili ya ugonjwa wake mwenyewe wa wasiwasi, Bwana. Yuko karibu kuchanganyikiwa. Mungu, naomba kwamba Wewe utampa shauku ya moyo wake. Mponye mateso yake, na umpe afya. Katika Jina la Yesu, ninaweka maombi haya ya imani juu yake. Amina.

Mungu akubariki, dada. Nenda zako, amini Yeye atakuponya. Mungu akubariki.

Bwana, kwa ajili ya wokovu wa wapendwa wake. Ninaomba kwamba utamjalia haja yake, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini sasa, dada, kwamba unapokea hilo, ndipo ni lako. Ukiamini, halina budi kutimia.

Kwa ajili ya Ndugu yetu Ted Dudley. Habari yako? Nautakia heri moyo wako. Umeruka kwa ndege kote kutoka Phoenix, Arizona. Je, kuna joto huko nje...?...

Mama huyo, hapa, aliponywa kutoka kwenye mkutano wangu. Alitoka wapi? Je, unatoka Phoenix, mama? Wewe si wa kutoka... Ulikuwa huko Phoenix, kwa ajili ya mkutano.

Unataka akufanyie nini, Ted? [Ndugu huyo anasema, "Aniondolee pumu."—Mh.] Akuondolee pumu. Mungu akubariki!...?...

²³² Mungu Mpendwa, kwa kuwa ndugu huyu wa thamani amekuwa msaada kwetu, Bwana, na kwa sababu ya watu walio na mzigo. Ninaomba kwamba Utamsaidia leo hii. Akitoka huko mbali Phoenix, Arizona, apate kuombewa, kusimama kwenye mstari huu, kusikia Ujumbe, kumtia moyo. Bwana, ilionekana kama dhabihu kubwa. Ndivyo ilivyo.

²³³ Lakini malkia wa Kusini alikuja, kwa miezi mitatu, mgongoni mwa ngamia, kupitia jangwa la Sahara, kusikia hekima ya Sulemani. Na tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yuko hapa; Roho Mtakatifu yuko hapa, aliye mkuu kuliko Sulemani.

²³⁴ Bwana, naomba kwamba utamponya mateso haya ya mwili wake. Mpe shauku ya moyo wake. Jalia atembea katika njia iliyowekwa kwa ajili yake. Jalia wema wa Mungu ukae juu yake. Ninaomba baraka hii kwa ajili ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina.

Ted, unaporudi, nenda nao. Ni wako. Nakupa wewe. Nenda ukaupokee.

²³⁵ Ndugu George, karibu kila mtu anamjua George Wright. Ni wangapi wanaokumbuka hadithi hiyo, wakati alipokuwa akifa hivi majuzi tu? Madaktari wote walipita karibu naye. Nao mwili wake ulikuwa umevimba namna *hiyo*, kuganda kwa damu moyoni mwake. Madaktari kadhaa walikuwa wamemkatia tamaa. Nilienda kumwomba. Ndugu Funk, alikuwa hapa muda mfupi uliopita; ninaamini alikuwa pamoja nami, huko chini wakati huo. Nikaketi juu ya kilima kule chini, nikajifanya kana kwamba nilikuwa nikienda kuwinda.

²³⁶ Nataka kusema jambo hili kwa kanisa hili sasa, sina budi kuelezea mambo fulani ambayo yamekuwa yakiendelea. Mara nyingi mnafikiria ninawinda; siwindi. Huo ni udhuru wa kuwazuia watu wasinifuate. Sina budi kwenda huko kuwa peke yangu na Mungu. Sio wakati wote ninawinda, enyi marafiki. Naam, mimi huwinda, lakini sio—sio uwindaji wa aina hiyo!

²³⁷ Niliketi juu ya kilima. Nikajifanya, kwake, nilikuwa naenda kuwinda sungura. Nikazunguka moja kwa moja, nyuma ya nyumba, kisha nikainua mikono yangu kuelekea kwenye hiyo nyumba, na kuomba na kuomba. Akifa!

Roho Mtakatifu akazungumza nami usiku mmoja, “Mmoja wa wanaume hawa anatoka katika kanisa ambalo haliamani kwamba uponyaji ni sawa.”

²³⁸ Mhudumu fulani alikuja nyumbani kwake, si muda mrefu uliopita, na kujaribu kushindana nami kule kwenye mjadala. Wengi wenu watu hapa, mlikuwapo huko usiku huo. Mnaona, mtu huyo karibu arukwe na akili. Sasa anajaribu kunitafuta apate Roho Mtakatifu. [Ndugu Wright anasema, “Loo, anasema mimi ndiye rafiki bora sana aliye naye, hata hivyo, ndugu.”—Mh.] Wazia hilo.

Mtu aliyesimama hapo kufanya mjadala, akasema, “Kwanza, nataka kukuambia, wewe ni wa ibilisi.”

Nikasema, “Nimekusamehe, kwa sababu hujui unalozungumzia.”

Kwa hivyo basi akageuka na kusema, “Najua una Roho wa Kristo.”

Nikasema, “Sasa, nilikuwa ‘ibilisi,’ dakika chache zilizopita, kisha ni ‘Kristo’ sasa. Ni yupi? Unaona?” Mnaona? Kwa hivyo sasa, wao, mambo mabaya sana yametokea.

Mtu *huyu* amelala pale, akifa. Naye mtu huyu akamcheka, akasema, “Sasa nenda kamtafute mponyaji wako wa Kiungu.”

²³⁹ Nami nilikuwa huko Lexington, Kentucky, ambako mwanamke mmoja aliponywa kansa. Na katika ono, Bwana alinionyesha, nikirudi, asubuhi hiyo yapata saa kumi na moja. Alinionyesha hilo. Kasema, “Utapeana mkono na Ndugu George Wright, akipitia maskanini, na kuja hapa juu na kukupa mkono. Naye yule mtu ambaye alimdhiki, atachimba kaburi lake.” Sikujua, sikujua alichimba makaburi.

²⁴⁰ Nikampigia simu Dada Wright. Hapana shaka yuko hapa mahali fulani. Naam. Nikampigia simu Dada Wright. Nikasema, “Nina BWANA ASEMA HIVI.” Kweli. Hayo ndiyo aina ya maono ninayotaka kuona tangu sasa na kuendelea. Ninapomtabiria mtu kitu, kinarudi. Nikasema, “Ndugu George atachimba kaburi la mtu huyo, au atakuwa kwenye kaburi la huyo mtu anayemdhiki. Naye atakuja maskanini, nami nitampa mkono.” Hilo donge la damu likamwacha Ndugu George.

²⁴¹ Ndipo yapata mwezi mmoja au miwili, baada ya hapo, nilikuwa nimerudi. Naye sikuzote, sikuzote bila kukosa, huwa anakuja *hivi*. Lakini, asubuhi hiyo, alikuja *hivi*. Nilikuwa na wasikilizaji. . . Nikasema, “Angalia, angalia, angalia! Huyu hapa anakuja, papa hapa, mnaona, sawasawa kabisa na vile Yeye alivyosema.”

²⁴² Huyu hapa, leo. Hiyo imekuwa... [Ndugu Wright anasema, “Miaka tisa.”—Mh.] Miaka tisa iliyopita. [“Nilikuwa na madonge tisa ya damu yaliyosalia.”] Madonge tisa ya damu, miaka tisa iliyopita.

²⁴³ Jambo lingine, nilisikia kwamba Dada Hickerson... Je, Ndugu Hickerson yuko hapa leo? Kwamba ana nafuu. Hilo ni sawa. Alikuwa na madonge kadhaa ya damu, pia, mguuni mwake.

Sasa ana baridi yabisi mkononi mwake.

²⁴⁴ Huyu alikuwa ni binti yake, Dada Hattie ameketi pale pale, ambaye nilishuhudia juu yake muda mfupi uliopita, ambako ile huduma mpya ilitenda kazi mara ya kwanza. Hiyo ni kweli, Dada Hattie. Sijui kama wale wavulana wako ndani asubuhi ya leo? Wako pamoja nawe? [Dada Hattie anasema, “Huko nyuma.”—Mh.]

²⁴⁵ Hao wavulana wako wapi? Hao hapo wote wawili wamesimama moja kwa moja huko nyuma. Hao hapo wale wavulana wawili ambao mama yao alipata ninii yake... Inua—inueni mikono yenu, wavulana, wapate kuona ninyi ni nani. Sawa. Wamesimama nyuma pale. Ajabu, sivyo, Orville? Hakika ndivyo. Vema.

²⁴⁶ Ndugu George. [Ndugu Wright anasema, “Unanijua, Ndugu Bill. Ninaamini.”—Mh.] Najua unaamini. Na najua mara nyingi, nimelala mle chumbani mwako, usiku, nikiangalia nje dirishani, nikisikiliza, maskini ndege mwigo. Siku moja itatubidi kuvuka ng’ambo ya pili, Ndugu George. Hadi wakati huo, Mungu awe pamoja nasi. Najua atafanya hivyo wakati huo. “Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya. Wewe u pamoja nami.” Ono lile, hapa si muda mrefu uliopita, wakati nilipowaona hao wazee wakigeuzwa kuwa vijana tena, hivyo ndivyo nitakavyokuona siku moja.

²⁴⁷ Baba yetu wa Mbinguni, mpe ndugu yetu shauku ya moyo wake. Mponye hii baridi yabisi. Anazeeka, Baba. Ninaomba kwamba utamsaidia. Msaidie Dada Wright, Edith mdogo, na familia yote kule chini. Dada Hattie, watoto wake, wapendwa wao wote, kuwa pamoja nao, Baba. Jalia haja hii, kama ninavyoomba katika Jina la Yesu. Amina.

[Ndugu Wright anasema, “Nitakuwa na umri wa miaka sabini na tisa.”—Mh.] Sabini na tisa. Mungu akubariki, Ndugu Wright, akupe siku nyingi zaidi. Bwana asifiwe.

²⁴⁸ Ndugu Daulton. Jamani, jamani! Huyu hapa ndugu ambaye amekuwa wa thamani kwangu. Nitawaambia kilichotokea. Sina wakati wa kuyapitia hayo. Mkewe anajua. Kasema, “Alikuwa yuafa.” Mshtuko wa moyo, sivyo, dada? Basi, hapo kabla, Bwana alikuwa amempa ndoto, nayo tafsiri ikaja. Wakati mshtuko wa moyo ulipompata, alisimama moja kwa moja mbele yake, akasema, “Naukataa huu.” Mungu alikuwa amempa

ndoto kwamba itakuwa hivyo, ndipo tafsiri ikaja. Naye daktari alikuwa akifikiri huyu mtu alikuwa akifa wakati huo, huyu hapa hai, leo hii.

²⁴⁹ Bwana Yesu, kwa ndugu yetu wa thamani, ameendesha motokaa mwendo mrefu kuja kwenye mkutano huu asubuhi ya leo. Nyonga yake ni mbaya. Kama vile gari tu, Bwana, viungo vinaanza kudhoofika, kufifia. Lakini, Ee Bwana, uwe Nguvu zake. Wewe ndiwe Nguvu zetu. Ziba sehemu hii iliyolemazwa nyongani mwake. Ziba kila sehemu dhaifu, Bwana. Na umpe ndugu yetu mpendwa uponyaji wake, ninapombariki katika Jina la Yesu Kristo, Mwana Wako. Amina.

Mungu akubariki, Ndugu Daulton. Ndivyo itakavyokuwa.

²⁵⁰ Vema, dada, Bwana anaweza kukufanyia nini? [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mbona, Dada Daugherty. Huyu ni Betty? [“Ni mimi.”] Mbona, Betty, nakutakia heri!

²⁵¹ Ni nani kwenye maskani hii asiyemjua Betty Daugherty? Mara ya kwanza maskini huduma yangu ilipopata kufanya kazi, ilikuwa juu ya mtoto huyu. Ni wangapi wanakumbuka hayo? Mnaona?

Betty alikuwa na ugonjwa wa ngoma ya Mtakatifu Vitus. Naye alikuwa mahututi sana hata hakutenda kama mwanadamu. Hakuna daktari angeweza kumfanyia lolote.

²⁵² Nami nilikwenda St. Louis. Kanisa hili lilichanga pesa, nami nikakopa koti la mtu fulani. Nao wakapata dola kumi na moja juu, ili mimi niende kumwomba huyu msichana mdogo. Alikuwa msichana mdogo tu, karibu kama—karibu kama huyu msichana mdogo anayeketi papa hapa, mtoto mdogo wa kike. Nami nikakaa... Ndugu Daugherty yuko hapa? Hayupo hapa. Basi nikaomba na kuomba na kuomba; nisingeweza kufikia popote. Ndipo hatimaye, huku nimeketi nje kwenye gari la Ndugu Daugherty, nikaona ono la yale waliyopaswa kufanya.

²⁵³ Naye akafuata hilo ono sawasawa na vile Bwana alivyosema wafanye. Ninaamini, ilikuwa kinyume kidogo na mawazo yake, wakati huo. Lakini alifanya vile hasa Bwana alivyosema wafanye, ndipo Betty akaponywa. Mara ya kwanza nilipomwona, jinsi... Kasema, “Babu Daugherty kwenye ncha moja ya kitanda; Ndugu Daugherty, hiyo nyingine. Kisha kumwacha achukue kitambaa na kunawa uso na mikono ya huyo mtoto mchanga, na kadhalika.” Wakati nikiendelea na sala “Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe.”

Naye Betty sasa ameshikwa na watoto wa jicho. Nikapata kumuomba tu mu—muda mfupi uliopita, nyuma ya jengo, huko Chautauqua.

²⁵⁴ Betty, kipenzi, hebu tupitie haya kwa uangalifu sana sasa. Nataka kuushika mkono wako. Je, wewe ni kipofu, kabisa, Betty?

[Dada Betty Daugherty anasema, “Hapana.”—Mh.] Unaweza kuona tu mwanga wa mchana na kuingia kwa giza. Una umri gani sasa, Betty? [“Ishirini na miwili.”] Ishirini na miwili. Alikuwa na yapata miaka saba au minane, wakati huo. Dada Daugherty, umekuwa na mvuto mgumu, sivyo? Unajua, Betty, sikuzote nimeamini kwamba Mungu alikuwa na jambo fulani kwako kufanya. Ninaamini hiyo ndiyo sababu imekuwa hivi kwako. Nami—nami naamini ya kwamba adui amefanya kitu hiki kiovu.

255 Sasa, unajua, Betty, Dada, kama ningalikuwa na nguvu za kufikia mle ndani na kuwashika hao watoto wa macho na kuwatoa, ningefanya hivyo. [Dada Betty Daugherty anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Sina.

256 Lakini, Betty, kile nilichokwambia mara ya kwanza, hicho ni kweli; wakati ninapoketi hapa, na mimi na wewe, kama ndugu na dada katika Kristo. Ndugu Daugherty, baba yako wa thamani, ndugu mpendwa tu kama niliyewahi kuwa naye; mama yako mpendwa hapa. Nimeishi nyumbani kwenu, nanyi mkashiriki chakula chenu pamoja nami, na—na kila kitu. Umekuwa kama—kama kwamba kweli ulikuwa dada yangu. Nami nisingeweza kuwa mwaminifu zaidi ya vile ningekuwa pamoja na Delores anayeketi hapa nyuma.

257 Sasa, Mungu aliahidi jambo hili, Betty. Nataka kupata yote... Baba yako, akiwa mhudumu, wewe ukiwa umekulia katika familia inayowaomba wagonjwa. Bila shaka, umeombewa, mara nyingi. Imefika mahali ambapo, wakati mwingine tunapita tu juu yake, na huku na huku. Nasi kidogo tu—tu—tunapoteza thamani yake. Unaona ninachomaanisha? [Dada Betty Daugherty anasema, “Amina.”—Mh.]

258 Jamani, umekuwa msichana mzuri, mrembo, Betty. Ni aibu kuona macho yako yakiendelea hivyo. Je, Meda bado yuko humu jengoni? Mke wangu alitaka kukuona. “Nataka amuone Betty, jinsi amekuwa msichana mrembo.” Betty, ulikuwa maskini msichana mdogo, mrembo. Sikuzote umekuwa msichana mzuri.

259 Sasa je, kuna kitu chochote maishani, ambacho umekosea, Betty? Sasa, kama tu vile daktari angechunguza mwi—mwili wako wa kawaida, nataka kuitazama nafsi. Umemkosea Mungu, mahali popote, Betty? Kama umemkosea, ungama tu Kwake, “Bwana, kama utanijalia kulipitia tena, nataka... nitafanya tofauti.” [Dada Betty Daugherty anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndiyo, anaweza.

260 Jamani! Ni jambo la kushangaza mno. Hebu tuliwazie hivi. Sasa, sikujua kwamba Betty Daugherty angekuwa kwenye mkutano huu. Lakini wa kwanza, kwenye ule upambanuzi wangu mwingine, alikuwa ni Betty Daugherty. Hili hapa, limejirudia tena, kwenye mkutano wa kwanza juu ya hili.

²⁶¹ Alijua papo hapo kile nilichokuwa nikizungumzia. Sitaki kuanzisha upambanuzi huo tena, maana, mstarini. Lakini alisema kile alichopaswa kusema hivi sasa. Alijazwa na Roho Mtakatifu, wakati akiwa, huko St. Louis. Kama msichana tineja, mtoto, labda amefanya mambo asiyopaswa kufanya. Lakini, ni nani hajawahi? Nani hajawahi? Kama si neema, sisi sote tumepotea. Na ikiwa uko tayari kukiri makosa yako, Mungu ni mwenye haki, kusamehe makosa yako.

Ninainua imani yangu sasa.

²⁶² Bwana, namleta msichana huyu Kwako. Ninaweka mikono yangu juu ya jicho lake. Ninakemea watoto hawa wa macho, na ninaamini kwamba Betty ataona tena. Jalia Nguvu zilizoyafungua macho ya kipofu Bartimayo, zimpe Betty kuona tena, ninapoomba dua hii, wakati imani ikiwa juu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Naomba nipeane mikono na dada yangu tena, mahali fulani, leo, kesho, au wakati wowote ule tena. Nayo hayo macho maangavu yataniona, na kusema, “Ndugu Branham, ninaweza kuona vizuri kama nilivyowahi kufanya katika siku zangu zote za shule.”...?... Na iwe hivyo.

Unaamini hayo, Dada Daugherty? [Dada Daugherty anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi itakuwa hivyo....?...

²⁶³ Bwana, katika Jina la Yesu, Mwana wa Mungu, mpe dada yetu shauku ya moyo wake, anaposimama akiinua mkono wake. Jalia Nguvu zilizomponya Betty Daugherty, mara ya kwanza, na hii pia mara ya pili. Jalia zimponye dada yetu, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁶⁴ Ndugu. [Ndugu huyo anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndugu yetu anataka kuokoka. Unamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako binafsi? [“Naam.”] Unaamini kwamba Yeye alikufa kwa ajili yako, na kufufuka tena? [“Naam.”] Sasa unamkubali kama Mwokozi wako binafsi? [“Naam.”]

²⁶⁵ Katika Jina la Yesu Kristo, jalia kila swali la dhambi liondoke kwenye dhamiri ya mtu huyu. Ndugu yetu na awe leo, tangu sasa na kuendelea, bila shaka Mkristo, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁶⁶ Ligeukie kusanyiko hili na kusema, “Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu.” [Ndugu huyo anasema, “Ninamkubali Kristo kama Mwokozi wangu.”—Mh.] Ana furaha sana dhambi zake zimesamehewa na Damu ya Yesu Kristo. Hiyo ndiyo tunayopenda, amina, tiba maradufu.

²⁶⁷ Bwana, mpe huyu mwanamke hakikisho la wokovu wake, na shida zake zote, Yesu, na ajaliwe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Nenda. Umeupokea. Nenda ukiamini sasa. Usiruhusu... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...?...

268 ...kwamba nimetimiza mengi zaidi, asubuhi ya leo, kwa Ujumbe ambao nimekuwa nao na mambo ambayo nimejua. Nimefuata lile agizo, zaidi, kuliko nilivyotimiza katika miaka mitano iliyopita, kwa sababu nimepata kiini cha mapenzi ya Mungu.

269 Sasa, linaweza kuwa jambo gumu kwangu kubadilisha kutoka huduma moja kwenda kwa nyingine. Lakini, sio kubadilisha huduma. Ni kuipeleka huduma ile ile katika mazingira ya juu zaidi. Ni agizo la asili. Vitu hivi vingine vyote vimekuwa vikijengwa juu ya hiyo. Sasa ndiyo wakati.

270 Kwa moyo wangu wote, ninaamini kwa ajili ya kila mtu ninayemwombea. Ninaamini watapata afya. Na kwa ushahidi wote tulio nao, kila kitu ambacho Mungu ameonyesha, cha mwaka baada ya mwaka, cha thibitisho lisiloweza kukosea, cha Biblia kuishi tena, basi ingewezaje kushindwa? Kamwe haiwezi kushindwa.

271 Sasa, kuna njia moja tu ya kuifanya ishindwe, hiyo ni, wewe kutoiamini. Kama Yesu angesimama hapa Mwenyewe na angekuombea, na kupitia tendo lile lile ambalo tumepitia asubuhi ya leo, hakuna cha zaidi kingalitukia. Au, kama ungeamini kwa hicho kipimo cha imani, kwamba, hakuna cha zaidi kingeweza kutokea kuliko kile kitakachotokea, kama ukiamini kwa kipimo kile kile cha imani. Kwa sababu, mimi ninamwakilisha Yeye tu. Mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, mtu tu kama ulivyo wewe, mwanadamu tu. Lakini Mungu hana budi kuwa na mlango mahali fulani. Naye amethibitisha hilo kwa Neno Lake. Amelithibitisha kwa huduma. Amelithibitisha kwa Malaika wa Bwana. Nalo hili hapa. Sasa ni juu yetu, kuliadini.

272 Sasa kumbukeni, kama tu mtoto. Kama kumekuwako na mateso, usiyaone tena. Iwapo kumekuwana ugonjwa, haupo tena. Puuza tu dalili yoyote, kitu chochote ambacho ni kinyume na kile kilichoulizwa. Mara nyingi... Kila mtoto amjiaye Mungu, hana budi kujaribiwa. Tunajaribiwa, kuona kama tunaamini hilo, au la. Nawe utakuwa na vita na matatizo, lakini kumbuka, tuko kwenye maandamano yetu.

273 Mungu awabariki. Ninawapenda. Na mimi, kwa msaada wa Mungu, natumaini ataniruhusu niwatumikie, kama mtumishi Wake, kwa miaka mingi, mingi ijayo, ndiyo maombi yangu. Niombeeni.

Na sasa kumbukeni, usiku wa leo, *Mathibitisho Matano Yasiyoweza Kukosea Ya Kanisa La Kweli La Mungu Aliye Hai*. Hadi wakati huo...

Na tusimame, kwa miguu yetu, kwa muda mfupi.

274 Loo, kuna ibada ya ubatizo? [Ndugu Neville anasema, "Naamini ipo. Hebu tuone kama tunaweza."—Mh.] Loo, ibada ya ubatizo! ["Ni watu wangapi kwa ubatizo?"] Watu wa ubatizo,

mko hapa? Inua mkono wako, mtu yeyote kwa ubatizo. [“Kuna mtu.”] Moja, mbili tatu . . . Naam. Samahani sana, sana marafiki.

²⁷⁵ Sasa, kwa wale ambao hawana budi kuondoka, nitawaruhusu waende. Wengine wao wabaki kwa ajili ya ubatizo, wanaotaka. Tutakuwa na ibada ya ubatizo, kwa muda mfupi tu.

²⁷⁶ Baba Mungu, waruhusu waondoke wale ambao inawabidi kwenda, na baraka Zako, baraka Zako. Neema Yako na iwe juu yao. Tukikushukuru kwa yote yaliyotimizwa asubuhi ya leo, tunapoondoka kwenye ule mlima, tukianza kupanda juu. Bwana, naomba tupitie kwenye kila milki ya ngazi, mpaka tuufikie U—Ufalme wa Mungu. Tujalie, Bwana. Kuwa pamoja nasi sasa. Tusamehe dhambi zetu, wale ambao wanakaa sasa kwa kubatizwa wapate ondoleo la dhambi yao. Katika Jina la Yesu Kristo, mambo haya na yajaliwe.

²⁷⁷ Tukusanye pamoja tena, usiku wa leo. Nguvu Zako na baraka Zako na ziwe juu yetu, usiku wa leo. Na kuwe na usiku mzuri usiku wa leo. Wengi waliochanganyikiwa na wanyoshwe, usiku wa leo. Utujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Vema. Mwaweza kuketi sasa mkitaka, wakati tukijiandaa kwa ajili ya ubatizo. 

60-0911M Kama Nilivyokuwa Pamoja Na
Musa, Ndivyo Nitakavyokuwa Pamoja Na Wewe
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org